




**TLS:** Wakili aliyepigana mahakamani ni 'kishoka'

UKURASA 2


Nipashe
Spotika
WACHEZAJI WA 5 WALIOPASWA KUWEPO TUZO YA EPL 2023 UK. 12-13
MAKOCHA 5 WALIOKUMBWA NA RUNGU LA FA ENGLAND
ISIKUPITE
POCHETTINO

UKURASA 11

ISSN 0856 • Na. 0581325

# Nipashe

Jumatatu Mei 29, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

The ... ital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



# HAIJAISHA

• **Mayele** afunga goli la ajabu, vurugu zaibuka, waziri athibitisha kifo, majeruhi 30... *Endelea ukurasa wa 24*

## YALIYOMO



UKURASA WA 3

### ALIYEMTOBOA MKE WAKE KWA BISIBISI AKAMATWA

JESHI la Polisi mkoani Arusha limemkamata mtuhumiwa Isack...

UKURASA WA 7

### MUHIMBILI KUPANDIKIZA FIGO KWA KUTUMIA ROBOTI

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH) inajipanga kuanza upandikizaji wa figo kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya...

UKURASA WA 8

### WAUSIFU UTEKELEZAJI MRADI BOMBA LA MAFUTA

WABUNGE wamesifu mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika ya Mashariki...





Wajawazito wa Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga wakishiriki mbio za Mamathon jana zilizoandaliwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

## Mbio za wajawazito zageuka lulu

UKURASA 3



## Waendesha bodaboda walivyouawa kikatili kichakani usiku

UKURASA 2

**MICHEZO** **ROBERTINHO KUIANDAA SIMBA YA MAKOMBE** UK.24

**KATUNI** UK.6

# Waendesha bodaboda wauawa kikatili usiku

**Na Vitus Audax**

WATU wanne wakiwamo waendesha bodaboda watatu wanaokadiliwa kuwa na umri wa kati ya miaka 26 na 30 wameuawa kikatili kwa kushambuliwa na kuchomwa sehemu mbalimbali za miili yao kisha pikipiki zao kutelekezwa katika vichaka nje kidogo na Kijiji cha Nyakiswa, Kata ya Kyanyari wilayani Butiama mkoani Mara.

Shambulio hilo inaelezwa kufanyika na wahalifu ambao bado hawajafahamika na lengo lao halikufahamika kwa haraka usiku wa kuamkia Mei 28, majira ya saa tano usiku huku wakitokomea kusikojulikana na kutelekeza pikipiki tatu walizokuwa nazo waendesha bodaboda hao.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana baada ya kufika katika eneo la tukio, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi (CP), Awadhi Juma, alisema uchunguzi umeanza kufanyika na hakuna mtu yeyote aliyekamatwa kutokana na tukio hilo kufanyika nyakati za usiku.

Aidha, alisema watu walioshambuliwa na kuuawa ni wanne ambao wote ni wanamume bila kuwataja majina na kueleza kuwa kati yao watatu wametambuliwa kuwa ni waendesha bodaboda katika eneo la Kijiji cha Nyakiswa, lakini mmoja bado hajatambulika.

Akifafanua kuwa watu hao ni wahalifu na kuwa dhumuni lao bado halijafahamika kutokana na pikipiki walizokuwa nazo waendesha bodaboda hao kutokuchukuliwa na kukutwa katika eneo la tukio.

"Watu hawa wanaonekana walishambuliana kwa muda mrefu kutokana na eneo husika kukutwa na dalili za purukushani ndipo waendesha bodaboda hao walipo zidiwa kwa kuchomwa na vitu vyenye ncha kali vinavyosadikiwa kuwa silaha za jadi hadi kuwasababishia mauti," alisema CP Awadhi.

Mkuu wa Wilaya ya Butiama, Rodovick Kahegele, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu alikemea vikali vitendo vya namna hiyo na kuwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi katika kuwabaini wahusika ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Katika kipindi cha mwezi Mei, zaidi ya matukio manne ya mauaji ya kutumia silaha za moto pamoja na jadi yametokea katika maeneo mbalimbali mkoani Mara hali iliyosababisha Jeshi la Polisi nchini kutuma kikosi maalum cha operesheni kikiongozwa na CP Awadhi katika mikoa ya kipolisi Mara na Tarime Rorya, kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kusaka wahalifu ambao wamekuwa wakitekeleza matukio hayo.

Aidha, alisema kikosi hicho kimefanikiwa kuwakamata watuhumiwa sugu 21 wa uhalifu wakiwamo waliofanya mauaji ya mfanyabiashara wa madini mkoani humo, daktari Isack Daniel yaliyotokea Mei 3, mwaka huu.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Missenyi**
**Kituo cha Gera Mkoa wa Kagera**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 09/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ANISETI ARISTIDES WA KATENDAGURO.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ARISTIDES ATHANAS RUHIKULA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanatakiwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 06 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateulliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia:- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 25 mwezi 05 mwaka 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Missenyi**
**Kituo cha Gera Mkoa wa Kagera**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 06/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU BUCHARD KATTO MTUNGI WA GERA.**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RAYMOND KATTO MTUNGI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanatakiwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 01 Mwezi 06 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateulliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia:- Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 05 mwaka 2023



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitoa heshima za mwisho kwenye jeneza lenye mwili wa mbunge wa zamani wa Butiama na Musoma Vijijini, Wakili Nimrod Mkono viwanja vya Karimjee mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# TLS: Wakili aliyepigana mahakamani 'kishoka'

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kimepigilia msumari kuwa aliyedaiwa kuwa wakili na kuzua taharuki katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akidaiwa kuzuia wateja wake wasikamatwe, ni 'kishoka' ambaye amefanya kazi ya uwakili tangu mwaka 2019.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Rais wa TLS, Harold Sungusia, alisema baada ya kupokea taarifa kuhusu mtu huyo, walifanya kikao cha dharura na kuamua kuteua kamati teule ya uchunguzi wa kitaaluma wa tukio hilo na ilibaini kuwa mtu huyu anayejulikana kama Baraka Mkama sio wakili.

"Kamati hiyo ya watu wanne ilifanikiwa kumhoji mhusika kufanya mazungumzo na Jeshi la Polisi, uongozi wa mahakama pamoja na baadhi ya mawakili waliokuwa na taarifa za tukio hilo.

"Kamati pia ilipitia mfumo wa usajili mawakili ili kujiridhisha kuhusu taarifa za mtu huyo na katika mahojiano, Mkama alikiri kuwa yeye sio wakili ingawa amekuwa akifanya kazi kama wakili tangu mwaka 2019," alisema Sungusia.

"Katika mashauri aliyokuwa akiyasimamia akiigiza kama wakili, alikuwa akiwatoza wateja wake zaidi ya shilingi milioni tatu kwa kesi. Kwa hiyo, tumejiridhisha pasipo na shaka kwamba Baraka Mkama sio wakili na sio mwanachama wa TLS."

Sungusia alisema TLS itashirikiana na vyombo vya dola na vya utoaji haki ili kuhakikisha kuwa hatua stahiki za kisheria zinachukuliwa dhidi yake pamoja na watu wengine kama yeye katika kukomesha tabia hiyo ambayo inaelekea kuenea maeneo mengi nchini.

Alisema tayari wamepata taarifa muhimu za ziada kuhusu mtandao wa watu wasio mawakili wanaofanya kazi za uwakili (vishoka) na kulazimika kuiongezea muda kamati tendaji hiyo iliyoundwa ili kuchunguza zaidi mtandao huo hadi keshokutwa na kutoa taarifa zaidi. Pia Sungusia alisema TLS imekamilisha kuunda kikosi kazi maarufu kwa jina la Anti-Vishoka Taskforce kitakachofanya kazi ya kudhibiti watu ambao hawastahili kufanya kazi za mawakili.

Aliwakumbusha wananchi na wadau wake ikiwamo mahakama kuhakiki taarifa za watu wanaoruhusiwa kufanya kazi za mawakili kwa kutumia mfumo wao wa utambuzi wa mahakama unaojulikana kama e-wakili, ili kulinda na kusimamia maslahi ya mawakili, kulinda na kuwatetea wananchi dhidi ya vishoka hao na kwamba kufanya hivyo kutalinda hadhi na heshima ya mawakili.

"Na hii inatupa picha ngumu zaidi kuwa mtu anatetea watuhumiwa na wanaachiwa huru wakati yeye mwenyewe ni kishoka, tena anawatetea dhidi ya wakili wa serikali ambaye ni mbobevu kwenye sekta hiyo, inatupa taswira nyingine kwamba huu ni uhalifu wa hali ya juu ambao tunapaswa kushirikiana na vyombo vingine kumaliza hili tatizo," alisema Sungusia.

Alisema wameamua kufuatilia zaidi ili wafahamu na mawakili wengine aliokuwa anaingia nao mahakamani mtuhumiwa huyo na kama na wao walikuwa wanafahamu ni kishoka au la.

"Na kama walifahamu kama ni kishoka walichukua hatua gani, kama hawakufahamu ni kwanini hawakujiridhisha kwamba huyo ni wakili. Tutakuwa wakali kidogo katika hili kwa kupitia kamati ya nidhamu, ikitokea wakili unashindwa kubainisha uhalifu wa wewe pia kwa sehemu nyingine unapaswa kulaumiwa, kwa sisi mawakili tutahakikisha tunakuwa wakali kila mtu anamchunga wakili mwenzake kwa kuangalia kwenye mfumo."

Pia Sungusia alisema wanachunguza zaidi kufahamu ni kesi ngapi ambazo 'kishoka' huyo alisimamia na matokeo yake yalikuwa ni nini na kwamba kama kuna kesi ambazo bado ziko mahakamani wataongea na uongozi wa mahakama ili wazitambue na kupunguza athari.

Alitoa wito kwa mahakimu na majaji, wasiridhike na mtu anapotokea na kusema yeye ni wakili mpaka wajiridhishe kwenye mfumo kabla ya kuwaruhusu kufanya kazi hiyo.

Sungusia alisema pia wamebaini mtuhumiwa huyo aliwahi kufanya kazi ya ukarani katika kampuni mbalimbali na kuacha.

Alisema ili kumaliza tatizo hilo la vishoka, watapeleka maombi yao kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili sheria ya mawakili sura namba 341 hususani kifungu cha 40, 41, 42 viangaliwe upya.

"Kwa sababu tunahisi hata adhabu inayotolewa ya kifungo cha mwaka mmoja kwa vishoka bado ni ndogo sana ukilinganisha na ukubwa wa tatizo na athari zinazosababishwa na hawa watu," alisema Sungusia.

Mei 23, mwaka huu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Baraka Mkama, aliwazuia askari polisi wasikamate wateja wake muda mfupi baada ya kuachiwa huru wakikabiliwa na mashtaka ya kughushi stika za dawa mbalimbali kuzionyesha kuwa ni halisi wakati sio kweli.

Aidha, alikamatwa na polisi kwa mahojiano zaidi na kwamba hadi sasa hajaachiwa.

# Mbio za wajawazito zageuka lulu Korogwe

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa** KOROGWE

WAJAWAZITO zaidi ya 2,000 wamejitokeza katika mbio za Mamathon zilizozinduliwa na Mkuu wa Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, Jokate Mwegelo, kati yao saba walipata uchungu wakiwa katika mbio na kupelekwa hospitali.

Mbio hizo zilianza jana saa 12 alfajiri kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na kumalizika katika kiwanja cha Shule ya Msingi Mazoezi.

Dhumuni la Mamathon ilikuwa ni kutoa hamasa kwa wajawazito kujifungua salama na hatimaye kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Akizungumza na wananchi hao jana, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Mary Chatanda, alimpongeza Jokate kwa ubunifu mzuri alioufanya katika kujali afya ya mama na mtoto.

"Wananchi wa Korogwe mmepata jembe na mwendelee kumpa ushirikiano na sisi viongozi tutaendelea kumuunga mkono na katika hili ambalo amelianzisha aendelee nalo kwani linagusa maisha ya wajawazito na watoto moja kwa moja kulinda afya zao," alisema Chatanda.

Aliwapongeza wajawazito na wote walioshiriki na kumaliza mbio hizo kwa kuwa kufanya mazoezi kwa mjamzito kuna faida nyingi.

"Kupitia mbio hizi wapo wajawazito wamepelekwa hospitali tunawaombea wajifungue salama," alisema.

Chatanda aliwashakuru wajawazito hao kuendelea kushiriki mazoezi, kuzingatia lishe bora itakayowasaidia kujifungua salama ili kuisaidia serikali kufikia malengo yake ya kupunguza vifo kwa wajawazito na watoto wachanga.

Alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali za kufanya ujenzi wa vituo vinne vya afya, wodi ya dharura lengo ni kuhakikisha wananchi hao wanapata huduma kwa wakati bila ucheleweshaji. Chitanda aliwataka wajawazito kuacha tabia ya kujifungulia nyumbani na badala yake wafike katika vituo vya afya kwa kuwa kufanya hivyo itasaidia kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Aidha, alitaka hatua kali kwa wauguzi wa afya wanaokwenda kinyume na maadili ya kazi yao ili kuwapo kwa nidhamu ya kazi.

"Hivi karibuni tumesikia tukio lililotokea wilayani Kaliua mkoani Tabora la kuuliwa na kuchukuliwa viungo vya watoto wachanga. Ni tukio baya, tunalikemea na tunaiomba serikali iendelee kuchukua hatua kali kwa watumishi wasio na maadili kama hawa na waendelee kutoa mafunzo ya kuwakumbusha wajibu wao," alisema Chitanda na kuongeza kuwa;

"Nitoe wito kwa watumishi wa afya wote acheni kujihusisha na vitendo visivyo na maadili, tunafahamu kazi yenu ni wito hivyo mtende haki. Muwe na lugha nzuri kwa wagonjwa, mimi sitakubali kuona mjamzito ananyanyaswa muwahudumie kwa huruma mnapata mshahara kwa ajili ya wagonjwa bila hawa mshahara haupo acheni kuwakaripia wagonjwa," alisema Chatanda. Aidha, Chatanda alisema amepokea vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Korogwe na hiyo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuboresha huduma za afya ikiwamo ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Akizungumza na wananchi hao, Jokate alisema lengo la kufanya tukio hilo ni kuenzi yale yote ambayo Rais Samia ameyafanya kwa ajili ya kusaidia wanawake na watoto.

Alisema katika mbio hizo walitoa masharti kwa wale wenye ujauzito wa miezi kuanzia nane na kuendelea wasihudhurie mbio hizo kwa sababu wapo katika hali ya kujifungua wakati wowote.

Aliwapongeza wajawazito hao zaidi ya 2,000 waliojitokeza na wote walioshiriki kumaliza mbio hizo kwa kuwa kufanya mazoezi kwa mjamzito kuna faida nyingi.

# Aliyemtoboa mkewe kwa bisibisi akamatwa

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi mkoani Arusha limemkamata mtuhumiwa Isack Robartson (45), mkazi wa Sombetini jijini humo anayedaiwa kumpiga na kumjeruhi mke wake Jackline Mkonyi (38), mkazi wa Sombetini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Msejo, mtuhumiwa alikamatwa Himo mkoani Kilimanjaro.

Kamanda Msejo alisema mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa na upelelezi ukikamilika jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

"Jeshi linatoa onyo kwa watu wachache wanaofanya vitendo vya ukatili katika familia zao au sehemu nyingine. Waache mara moja.

"Niwaombe wananchi popote walipo wasifumbie macho vitendo viovu na waendelee kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za uhalifu katika maeneo yao ili kukomesha matukio hayo," alisema. Hivi karibuni akizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwa wazazi wake eneo la Sinoni Kata ya Darajambili jijini Arusha, Jackline alisema Mei 23, mwaka huu alitembelewa na mjomba wake ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Simiyu, Vicent Nicodemas.

Alisema ghafla mume wake alikwenda usiku majira ya saa 4:45 na kugonga mlango na baada ya kufunguliwa, aliingia chumbani na kuanza kutoa maneno mazito huku akimuuliza mchana alikuwa na nani.

Jackline alisema wakati akijieleza alijikuta akipigwa na mijeledi mgongoni na mume wake alichukua 'plaizi' kifaa cha gereji na kumwamuru afungue mdomo na kumng`oa meno japo aliona hiyo haitoshi na kuchukua kitu kingine chenye ncha kali na kumtoboa jicho moja.

**WILHELMSEN SHIPS SERVICE LIMITED**

[Company registration Number: 45072]
(UNDER VOLUNTARY LIQUIDATION)

**FINAL MEETING AND DISSOLUTION**
(Made under Section 345 (1) & (2) of The Companies Act Cap 212 RE 2019)

NOTICE IS HEREBY GIVEN to the GENERAL PUBLIC that WILHELMSEN SHIPS SERVICE LIMITED is undergoing Voluntary Liquidation and it has called for a Final Meeting and Dissolution of the Company which is intended to be held at the REGISTERED OFFICES OF THE COMPANY PLOT NO.2397, BLOCK 202, APEX TOWER, 6TH FLOOR, LUGODA STREET, GEREZANI, ILALA CBD, DAR ES SALAAM on the 31st _of _October_2022 at 1200 HOURS.

DATED THIS 15th DAY OF SEPTEMBER 2022

**INNOCENT RICHARD TAIRO**
**T/A TAIRO LAW OFFICE ADVOCATES**

1ST FLOOR, EXPORTERS BUILDING,
PLOT NO. 331/36, MKWEPU STREET,
DAR ES SALAAM.

Wilhelmsen Ships Service

Wilhelmsen Ships Service Ltd
VISIT Apex Towers, 6th Floor, Lugoda Street
POST PO Box 43013 Dar-Es-Salaam, Tanzania
TEL +255 22 2120654
TIN 101-747-794

WILHELMSEN SHIPS SERVICE LIMITED
[Company registration Number: 45072]

RE: NOTICE OF VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY

Notice is hereby given to the General Public that according to section 333 (b) of the Companies Act No. 12 of 2002

Members of the Company through a Special Members meeting dated 30th June 2021 have voluntarily decided to Wind Up the Company. It was further resolved that INNOCENT RICHARD TAIRO T/A TAIRO LAW OFFICE ADVOCATES of 1ST FLOOR, EXPORTERS BUILDING, PLOT NO. 331/36, MKWEPU STREET, DAR ES SALAAM be appointed as the Liquidator of the company.

This notification is issued to all who have a claim against the Company.

COMPANY SECRETARY

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA.147 YA MWAKA 2022**
**DAUD YOHANA CHILONGANI............MDAI**
**VERSUS**
**MELY MENENGO...............MDAIWA**

**KWA:**
**MELY MENENGO**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayomaelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Mpwapwa wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yoyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe **26/ 07/ 2023 Saa 3.00 Asubuhi.**

Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 15 ya Mwezi wa MEI,2023

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA CHATO**

**MAHALI LILIPO CHATO**

**MAOMBI / RUFAA NA. 23 MWAKA 2022**

**MISTA LINDA MAGULU.......MWOMBAJI/MRUFANI**

**DHIDI YA**

**PILI MBINZILE.........MJIBU MAOMBI/MRUFANIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: PILI MBINZILE**

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kuitwa/kusikilizwa tarehe 30 Mwezi May Mwaka 2023. Saa 2:30 asubuhi mbele ya **MH. A.M KAPINGA** Mwenyekiti wa Baraza.

Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa pamoja na utetezi/majibu yako ndani ya siku 21.

**AMRI** hii imetolewa leo kwa mkono wangu na Lakiri/Mhuri wa Baraza leo tarehe 18 Mwezi May Mwaka 2023.

MWENYEKITI

**INVITATION FOR BIDS (IFB)**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**TANZANIA NATIONAL PARKS (TANAPA)**

**Project: Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD)**

**(KfW Contract Reference No.:2012 66 451)**

**29th May 2023**

1. The Government of the United Republic of Tanzania has received a grant from the German State-Owned Investment and Development Bank (KfW) towards the costs of implementing the Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD), and intends to apply part of the proceeds towards payments under the contract for Construction of Rural Infrastructure (i.e., Socio-economic Infrastructures) in Nyerere National Park (NNP).

2. The Tanzania National Parks Authority (TANAPA) now invites sealed bids from eligible and qualified bidders for the construction works comprised of various rural socio-economic Infrastructures as shown in the table below:

| Package Number | Tender Number | Procurement Plan Number | Tender Description |
|---|---|---|---|
| 003 | MNRT/GOPA/KALDORMPP20 | PP 20 | Construction of a Dormitory Building, Water Towers and WMA Ranger Posts at Kalulu Subzone for the Nyerere National Park (NNP) – Lot 1 |
| | MNRT/GOPA/KALDORMPP21 | PP 21 | Construction of a Dormitory Building at Kalulu Subzone for the Nyerere National Park (NNP) – Lot 2 |
| | MNRT/GOPA/KALDORMPP22 | PP 22 | Construction of a Dormitory Building at Kalulu Subzone for the Nyerere National Park (NNP) – Lot 3 |
| 004 | MNRT/GOPA/ RANGERPP23 | PP 23 | Construction of a Patrol/ Ranger Post at Machungwa – Msolwa Subzone for the Nyerere National Park (NNP) |
| 005 | MNRT/GOPA/ KITARANGERPP24 | PP 24 | Construction of a Patrol/ Ranger Post at Kitanda – Ilonga Subzone for the Nyerere National Park (NNP) |
| 006 | MNRT/GOPA/ SAFARI7RANGERPP25 | PP 25 | Construction of a Patrol/ Ranger Post at Safari Five – Liwale Subzone for the Nyerere National Park (NNP) |
| 007 | MNRT/GOPABWALARUBADORMPP30 | PP 30 | Construction of Dormitory Building and Water Tower at Bwawa La Ruba – Liwale Subzone for the Nyerere National Park (NNP) |
| 008 | MNRT/GOPA/MSOLIKGSYHSEPP19 | PP 19 | Construction of two (2) Guest Houses for the Nyerere National Parks at Msolwa and Likuyu Sekamaganga Subzones |
| 009 | MNRT/GOPA/BOREHOLE/PP14 | PP14 | Construction of (1) Borehole at Miguruwe Sector Headquarters Selous Game Reserve and (3) Boreholes at Likuyu Sekamaganga, Ilonga and Kalulu Subzone at Nyerere National Park (NNP) |

***Note:***
- ***Bidders are allowed to submit offers for more than one package***
- ***All lots within a package must be included in the bid applicable to package number 003.***

3. Bidding will be conducted by means of the National Competitive Bidding (NCB) procedure with the qualification as specified in the KfW Guidelines for Procurement of Goods, Works and associated Services in Financial Cooperation with Partner Countries ("KfW Guidelines"

**https://www.kfw-entwicklungsbank.de/PDF/Download-Center/PDF-Dokumente-Richtlinien/FZ-Vergaberichtlinien-V-2021-EN.pdf).**

4. A complete set of the bidding documents **(in English)** is available to interested eligible Bidders upon the submission of a written application to the address below and upon payment of a non-refundable fee of **Tanzanian Shillings One Hundred Thousand only (TZS 100,000.00).** The method of payment is via bank deposit to the following account at **Tanzania CRDB bank - Account name: Selous Ecosystem Conservation and Development with Account number 0150555174201.**

The documents shall be sent by Courier (related costs to be covered by the interested Bidder) or physical pickup by the Bidders at ***Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.***

5. Bids in one original plus two paper copies and one digital copy, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below: **SECAD Project Manager, Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania** on or before Wednesday **5th July 2023 at 12:00 hours EAT.** Electronic bidding will not be permitted and late bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the bidders' or designated representatives and anyone who choose to attend at the address below on **Wednesday 5th July 2023 at 14:00 hours at MNRT Room No. L406.**

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT)**
**c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No.L406, PO Box 25295,**
**40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Contact: - SECAD Project Coordinator**
**Email: - SECADtenders@gopa-infra.de**

# CRDB yazidi kujitanua ikifikisha matawi 251

**Na Mwandishi Wetu,** KILWA

BENKI ya CRDB imefungua matawi mapya mawili mkoani Lindi, hivyo kufikisha jumla ya matawi 251 yanayotoa huduma nchini kote na kuifanya kuwa benki yenye mtandao mkubwa zaidi nchini.

Akizindua tawi la Benki ya CRDB wilayani Kilwa mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, aliipongeza benki hiyo kwa jitihada hizo na akaitaka iongeze juhudi za kuwaelimisha wananchi na kushusha riba ya mikopo inayotolewa ili kuwavutia wananchi wengi kutumia huduma za benki.

"Kwa idadi ya matawi mliyonayo, ninyi ndiyo benki inayowafikia wananchi wengi zaidi nchini. Ninawaomba mwongeze kasi ya kuwaelimisha wananchi huku mkiangalia namna ya kushusha riba ya mikopo mnayoitoa.

"Mkifanya haya ninaamini wateja wengi watahamasika kutumia huduma zenu. Ninyi mkianza itakuwa rahisi kwa wengine kuiga. Wananchi wakishawishika kutumia huduma za benki itasaidia kufanikisha malengo ya serikali ya kuongeza ujumuishaji wananchi katika huduma za fedha na uchumi kwa ujumla," Zainab alisema.

Mkuu wa Mkoa pia alisema sekta ya fedha ni muhimu kwa maendeleo ya taifa, hivyo kutakuwa na manufaa zaidi iwapo wananchi wengi watatumia huduma za benki, jambo litakaloirahisishia serikali kufahamu fedha zilizopo katika mzunguko zinaelekea wapi.

"Fedha ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya taifa. Hivyo ukuaji wa sekta ya hii ni muhimu sana katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Lakini, ili sekta ya fedha itoe mchango unaokusudiwa, inapaswa iwe imara, iwe na uwezo mkubwa wa kuwafikia wateja wengi mjini na vijijini.

"Benki zinatakiwa zizingatie mahitaji ya wananchi na ziwahamasishe wananchi kutambua umuhimu wa kutumia huduma za benki kwa maendeleo binafsi na ya taifa letu kwa ujumla wake. Kipekee kabisa ninawapongeza sana Benki ya CRDB kwa kuwa mstari wa mbele katika kufanikisha hili," Mkuu wa Mkoa alisema.

"Ni muhimu kwa wafanyabiashara, wajasiriamali na wateja wa kada nyingine kuchangamkia fursa hii.

Nitoe rai kwenu Benki ya CRDB kuweka masharti na vigezo nafuu ikiwamo kutoza riba ndogo ili watu wengi zaidi wajitokeze na kunufaika na mikopo mnayotoa na kuachana na mikopo ya mtaani ambako wanatozwa mpaka riba ya asilimia 50 na kujikuta katika matatizo yasiyo ya lazima," aliongeza Mkuu wa Mkoa.

Godfrey Rutasingwa, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Benki ya CRDB, alisema kuna fursa nyingi zinazopatikana katika matawi yao yote ambazo zinakidhi mahitaji ya kila mteja.

"Kwa sasa tunayo programu ya Imbeju inayotoa mtaji wezeshi kwa wanawake na vijana. Zaidi ya Sh. bilioni tano zimetengwa kwa ajili hiyo na zitaongezwa iwapo kutakuwa na uhitaji mkubwa.

"Wanawake na vijana ni kundi kubwa lakini limeachwa kidogo. Hivyo, benki yenu ya CRDB imeliona hilo na kulifanyia kazi. Karibuni katika matawi yetu mpate huduma za uhakika," alisema Rutasingwa.

Rutasingwa alizitaja fursa nyingine ni usalama wa kutunza fedha na urahisi wa kupata mkopo. Kuwapo Benki ya CRDB Kilwa kuna maana ya kuongeza urahisi wa upatikanaji wa mikopo kwa wananchi ikiwamo ya biashara na kilimo, hali itakayosaidia kuchochea ukuaji wa uchumi katika wilaya hiyo na za jirani.

Kwa wafanyabiashara hata wananchi, Rutasingwa alisema kwa kutumia huduma za CRDB wana uhakika wa urahisi wa kufanya malipo kupitia mifumo ya kidijiti. Alisema maendeleo ya teknolojia yamesaidia kurahisisha upatikanaji wa huduma na benki imewekeza kwa kiwango kikubwa katika mifumo hiyo ili kutoa huduma kwa wananchi wakati wote ikiwamo ulipaji wa kodi na tozo za serikali.

Mkurugenzi huyo alisema mteja wa Benki ya CRDB anaweza kupata huduma hizo kwa saa 24 akiwa mahali popote.

"Ukiwa mtaani, kuna mawakala wetu huko wanaotoa huduma mbalimbali na ukiwa nje ya nchi kuna internet banking na kadi zetu za ATM unazoweza kuzitumia. Tunafanya haya yote kuhakikisha tunakidhi matarajio ya wateja wetu," alisisitiza Rutasingwa.

# China yapendekeza kuimarisha ushirikiano zaidi na Afrika

**Na Mwandishi Maalum**

BEIJING - Waziri wa Mambo ya Nje wa China Qin Gang, amependekeza kuimarisha zaidi ushirikiano kati ya China na Afrika katika kuadhimisha Siku ya Afrika.

Akihutubia katika hafla hiyo, Qin kwa niaba ya Serikali ya China ameupongeza Umoja wa Nchi Huru za Afrika kwa kuadhimisha miaka 60 tangu kuanzishwa kwake, akibainisha kuwa Afrika imekuwa nguvu muhimu yenye ushawishi wa kimataifa na hadhi ya kimataifa inayopanda.

"Kuingia katika zama mpya ya kujenga jumuiya iliyo karibu zaidi kati ya China na Afrika yenye mustakabali wa pamoja, China na Afrika zinahitaji kuimarisha umoja na ushirikiano zaidi kuliko hapo awali," Qin alisema.

Alitoa wito kwa China na Afrika kulinda kithabiti haki na maslahi halali ya kila mmoja wao na kuimarisha zaidi uungaji mkono wa pande zote katika masuala yanayohusu mamlaka, maendeleo na heshima ya kila mmoja wao.

China na Afrika zinapaswa kuhimiza kikamilifu programu za maendeleo ya kisasa zenye sifa bainifu, Qin alitoa wito kwa pande zote mbili kuhimiza uoanishaji kati ya Pendekezo la Ukanda Mmoja, Njia Moja, Pendekezo la Maendeleo ya Dunia, Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika na mikakati mingine ya maendeleo ya nchi za Afrika na kuisaidia Afrika kuharakisha ukuaji wa viwanda, ujanibishaji na mseto wa kiuchumi.

Qin alisema China na Afrika zinapaswa kuhimiza kwa pamoja mageuzi ya mfumo wa utawala wa kimataifa, kulinda maslahi ya pamoja ya nchi zinazoendelea na kuendelea kuunganisha nguvu za nchi zinazoendelea.

Alitoa wito wa kuimarishwa zaidi kwa mabadilishano na kujifunza kwa kila mmoja miongoni mwa ustaarabu na kuharakisha utekelezaji wa Pendekezo la Ustaarabu wa Dunia barani Afrika.

Demeke Mekonnen Hassen, Naibu Waziri ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Ethiopia, na Christophe Lutundula, Makamu wa Waziri Mkuu ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, walihudhuria tafrija hiyo.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA Shughuli za Kupiga Mbizi**

**KUMB: ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0122**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za Ujenzi wa Gati na Kituo Cha Kupakilia katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa utojai wa huduma za:

**- Shughuli za kupiga mbizi**

**MAELEZO MAFUPI YA UPEO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Shughuli za Upigaji mbizi wa Baharini hadi kina cha mita 25
- Kukata nguzo za chuma kwenye maji
- Ufungaji wa vifaa vya Cathodic protection chini ya maji
- Kulehemu Tag Chini ya maji
- Urejeshaji wa kizuizi, mnyororo au Kamba ya nanga inapokatika
- Ukaguzi / kusafisha meli (Hull Inspection / Cleaning) inapihitajika

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa:

- Wasifu wa kampuni na uthibitisho wa rasilimali za kutosha za kifedha na zenye uwezo kusimamia kandarasi husika.
- Orodha ya uzoefu iliyo na historia ya ugavi / rekodi inayoonyesha uzoefu wa chini wa miaka mitano (5) katika kutekeleza huduma sawa za kupiga mbizi baharini kulingana na viwango vya kimataifa vya kawaida katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linalofanana.
- Maandalizi ya Taarifa ya Mbinu (Methos Statement) za Kuzamia ikiwa ni pamoja na tathmini ya vihatarishi kulingana na viwango vya mradi na Sheria za nchi.
- Maandalizi ya mpango mkakati wa kina wa Kuzamia kulingana na viwango vya mradi na Sheria za nchi.
- Maandalizi ya mpango wa Ubora (Quality Plan) kulingana na mpango wa Ubora wa Mradi, viwango vya mradi na Sheria za nchi.
- Maandalizi ya utaratibu wowote wa kupiga mbizi ili kuzingatia viwango vya mradi na sheria za nchi
- Uthibitisho wa Hati ya Mlipoa kodi ya kampuni kwa mwaka uliopita 2022
- Uthibitisho wa usajili wa biashara na leseni halali ya biashara kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili wa biashara na udhibitisho kutoka kwa taasis za udhibiti (TASAC).
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli Na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha ombi, maslahi unapendekezwa zaidi.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa barua pepe na viambatanishi: 20 MBs & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **tarehe 12 Juni 2023 , 1200 jioni Saa za Tanzania.**

Kichwa cha ombi kijumuishe nambari ya kumbukumbu kama ilivyoonyeshwa kwenye kichwa cha tangazo hili la EOI.

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA MAANDALIZI YA KAZI ZA UMEME KWENYE OFISI ZA MRADI.**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia Mafuta katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa:

**Kazi za Umeme kwenye Ofisi za Mradi.**

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

- Shughuli za Umeme zitakuwa kwenye eneo la bandari ya Tanga
- Kuunganisha na umeme wa TANESCO (kazi ifanyike kwa vibali vyote vinavohitajika kisheria)
- Kuunganisha umeme kwenye kontena 20 No. za ofisi na vifaa vya ofisini
- Kuandaa na kutengeneza MDB na DB, michoro ya nyaya (cable layout)
- Swichi ya Kubadilisha umeme wa TANESCO na jenereta 2 za 150kva
- Michoro itatolewa na BBN
- Michoro ya DB's itatolewa na BBN

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo.
- Uthibitisho wa Hati ya mlipa kodi ya kampuni ya mwaka uliopita 2022
- Uthibitisho wa usajili wa biashara na leseni ya biashara kwa Tanzania
- Uthibitisho wa usajili wa mkandarasi na udhibitisho kutoka kwa bodi za udhibiti / usimamizi (CRB, ERB nk)
- Ubora wa Kampuni na Sera ya HSE na cheti cha uthibitisho wa OSHA
- Kuzingatia kanuni za petroli na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) , unapendekezwa zaidi.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma , yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **Procurement@bbnjv.com . (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **tarehe 12 Juni 2023, saa 12jioni majira ya Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

TANGAZO

MCB BANK BETTER TOGETHER

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### KUTOKA TAARIFA YA FEDHA ILIYOKAGULIWA NA KUIDHINISHWA NA WAKAGUZI WA MAHESABU

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DISEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mwaka wa sasa 31-Disemba-2022 | Mwaka uliopita 31-Disemba-2021 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 313 | 237 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 9,556 | 7,805 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 18 | 34 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 41 | 30 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 5,302 | 1,002 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 64,087 | 44,676 |
| 12. Mali Nyingine | 3,095 | 3,576 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 856 | 829 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **83,268** | **58,189** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | 4,001 | - |
| 18. Amana za Wateja | 60,178 | 38,720 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 824 | 541 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 1,334 | 1,700 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27. Dhima Nyingine | 1,256 | 1,210 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **67,593** | **42,171** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **15,675** | **16,018** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | - |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 17 | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (19,923) | (18,508) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (331) | (1,387) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,675** | **16,017** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 577 | 523 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 434 | 382 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 19% | 28% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.7% | 1% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 106% | 115% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 77% | 77% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83% | 79% |
| - Ongezeko la Amana | 55% | 109% |
| - Ongezeko la Mali | 43% | 50% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Disemba-2022 | Limbikizo la Mwaka uliopita 31-Disemba-2021 |
|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 8,627 | 5,674 |
| 2. Gharama za Riba | 3,411 | 1,783 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **5,216** | **3,891** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 263 | 51 |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 1,936 | 1,359 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | 5 | 1 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,804 | 1,301 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 127 | 57 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 7,185 | 6,561 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 3,110 | 2,874 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 4,075 | 3,687 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(296)** | **(1,362)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | 36 | 25 |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(332)** | **(1,387)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(332)** | **1,387** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 58 | 55 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -5 | -22 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *-0.40%* | *-2.38%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *-2.11%* | *-8.66%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *104.29%* | *127.60%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *7.52%* | *7.94%* |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Disemba-2022 | Limbikizo la Mwaka Uliopita 31-Disemba-2021 |
|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (296) | (1,362) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| - Hasara katika Mali | 1,244 | 1,329 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (23,695) | (18,276) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 25,460 | 19,686 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (834) | 357 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (747) | 156 |
| - Kodi Iliyolipwa | (15) | (35) |
| - Mengineyo | (383) | (333) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **734** | **1,522** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| - Gawio Lililopokewa | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (315) | (218) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| - Mengineyo | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(315)** | **(218)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| - Mengineyo (Mtaji tangulizi) | 219 | 262 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **219** | **262** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Tas | 638 | 1,566 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 6,051 | 4,485 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 6,689 | 6,051 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Mtaji tangulizi | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (19,895) | 5,000 | - | 16,017 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (331) | - | - | (331) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | (17) | - | 17 | - |
| Nyingine | - | (11) | - | - | (11) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(20,254)** | **5,000** | **17** | **15,675** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (18,508) | - | - | 12,404 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (1,387) | - | - | (1,387) |
| Mtaji tangulizi | - | - | 5,000 | - | 5,000 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(19,895)** | **5,000** | | **16,017** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2022**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Chief Executive Officer) | ……………………. (Imesainiwa) | 26 Mei 2022 |
| Selemani Kijori (Head of Finance) | ……………………. (Imesainiwa) | 26 Mei 2022 |
| Patrick Mashalla (Head of Internal Audit) | ……………………. (Imesainiwa) | 26 Mei 2022 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani (Mwenyekiti) | ……………………. (Imesainiwa) | 26 Mei 2022 |
| 2/ Enna V. Mwakipesile (Mkurugenzi) | ……………………. (Imesainiwa) | 26 Mei 2022 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga wasahau matokeo nyumbani, wajipange kumaliza kazi ugenini

**JANA** taifa limeshuhudia tukio kubwa la mpira lililovuta hisia za mashabiki wengi wa soka ndani na nje ya nchi.

Wawakilishi Watanzania kwenye michuano ya CAF, Yanga walikuwa uwanjani kuumana na wapinzani wao kwenye fainali ya Kombe la Shirikisho, klabu ya USM Alger ya Algeria kwenye fainali ya mkondo wa kwanza.

Ni mchezo mgumu ambao ulikutanisha klabu bora kwenye michuano hiyo msimu huu ambazo ziliwatoa vigogo wengine na kufuzu kucheza hatua hiyo.

Kwa bahati nzuri, Shirikisho la Soka Afrika limeweka utaratibu wa kuchezwa mechi mbili katika hatua ya fainali, mechi ya nyumbani na mechi ya ugenini kabla ya kumpata bingwa wa michuano husika.

Yanga jana ilikuwa kwenye uwanja wa nyumbani kujaribu kuweka rekodi ya kutwaa ubingwa wa kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu na Taifa kwa ujumla. Kimsingi mchezo wa kwanza ambao ni sawa na dakika 45 za kipindi cha kwanza umeshapita, bado kuna dakika 45 za pili ambazo ni mchezo wa marudiano utakaochezwa Juni 3 nchini Algeria.

Kwa sasa wawakilishi wetu, Yanga wanapaswa kusahau matokeo waliyoyapata kwenye mchezo wa jana wa nyumbani na badala yake sasa waelekeze nguvu na akili zao kwenye mchezo wa marudiano ambao ndio utatoa bingwa wa michuano hiyo ya CAF kwa msimu huu. Kocha wa Yanga na benchi lote la ufundi, wana kazi nyingine mbele yao ya kuhakikisha wachezaji wao wanasahau matokeo waliyoyapata kwenye mchezo wa kwanza na sasa wauangalie mchezo wa marudiano.

Ni wazi matokeo ya mchezo wa kwanza bado hayaamui bingwa wa michuano hii, kwa sasa timu zinaenda kujiandaa kwa ajili ya mchezo wa marudiano ambao ndio hasa utatoa mwanga wa nani bingwa wa Kombe la Shirikisho msimu huu.

Wachezaji wa Yanga wajue bado kuna kazi mbele yao katika harakati za kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kwenye michuano hii ya CAF.

Hakuna ubishi msimu huu umekuwa msimu bora kwa soka la Tanzania ambalo limeshuhudia timu moja wapo katika Ligi Kuu ya soka Tanzania bara ikicheza hatua ya fainali ya moja ya michuano ya CAF.

Hii ni hatua kubwa sana, zipo ligi nyingi Afrika ambazo wawakilishi wake hawajavuka hata hatua ya makundi ya michuano ya CAF kuanzia ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika mpaka hii ya kombe la Shirikisho Afrika.

Wachezaji wa Yanga ni lazima watambue, kazi bado haijakamilika, kuna mchezo mwingine ugenini hivyo ni lazima kujiandaa kimwili na kiakili kuhakikisha wanaenda kufanya vizuri na ikiwezekana kutwaa ubingwa huu ili kuweka historia Tanzania. Wachezaji wasahau matokeo yao kwenye mchezo wa kwanza na wajiandae kwenda kupambana kama vile hakuna kilichotokea kwenye mchezo wao wa nyumbani, kwa kufanya hivyo kutawafanya wapambane na kubaki kwenye mstari wa kuelekea kwenye ubingwa wa Afrika.

Tunaamini Yanga wana nafasi ya kuchukua ubingwa huu kama wataendeleza makali yao kwenye viwanja vya ugenini kwa kupata matokeo mazuri yatakayoifanya iandike historia kwa kuwa timu ya kwanza kutwaa ubingwa wa Afrika.

Nipashe tunaitakia kila la kheri wawakilishi wetu hawa kwenye michuano ya CAF, tunaamini hakuna kisichowezekana kwenye mpira, mchezo wa marudiano wachezaji waelekeze akili na nguvu zao huko ili kufanya vizuri na kutwaa ubingwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Utaratibu kuingia uwanjani mechi kubwa uangaliwe upya

Na Adam Fungamwango

**KABLA** ya pambano la fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kati ya Yanga dhidi ya MC Alger ya Algeria, halijachezwa kulikuwa na patashika nguo kuchanika nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, kati ya walinzi wa mageti, askari polisi dhidi wa wananchi ambao walijitokeza kwa wingi kwenda kushuhudia mechi hiyo.

Picha mbalimbali zilionyesha, umati wa watu wakitaka kujaribu kuingia uwanjani lakini wakashindwa, pia kulikuwa na tukio la mashabiki hao hao kuvunja geti na kuanza kuingia uwanjani.

Tumeona pia Jeshi la Polisi likipambana na baadhi ya mashabiki ambao walikuwa wakiruka uzio na kutaka kuingia uwanjani. Wengine walikuwa wanafanikiwa, lakini baadaye gari lenye maji ya kuwasha lilianza kumwaga maji kwa ajili ya kudhibiti mashabiki walioanza kuwazidi nguvu walinzi wa getini.

Tayari ilisharipotiwa kuwa tiketi zote zilikuwa zimekwisha, hivyo moja kwa moja ilijulikana kama uwanja umeshajaa.

Kwa kawaida shabiki ni shabiki tu na anapaswa adhibitiwe, lakini inaonekana ni kama askari polisi na walinzi wa getini walishtukizwa na matukio hayo ambayo wao walidhani hayatoweza kutokea.

Sehemu yenye umati mkubwa kama huo kuna watu wa aina zote, watulivu na wakorofi, hivyo nadhani walinzi walipaswa kujipanga mapema kukabiliana na yaliyotokea kuliko walivyofanya baada ya tukio hilo.

Nilidhani baada ya polisi na walinzi kufahamu kuwa tiketi zote zilikuwa zimeuzwa wasingeruhusu mashabiki wasiokuwa na tiketi kuvuka barabara au kuusogelea uwanja, badala yake wangewazuia na kukaa mbali kando ya barabara.

Na yeyote ambaye angevuka barabara, basi angefanya hivyo huku akionyesha tiketi au kadi yake ambayo ingemruhusu kuingia uwanjani.

Kwa sababu tiketi zilikuwa zimeshauzwa hakukuwa na ulazima wa mashabiki kuwa karibu na uwanja au getini kama hawakuwa na tiketi za kuingia uwanjani.

Lakini kilichotokea, ni kwamba walinzi na askari waliwaacha mashabiki wakiwa wamezunguka uwanja, wengi wakiwa wamejazana magetini bila kujua kama wana tiketi au la.

Kitendo cha kuwaacha ina maana yalikuwa mawili, ama ni uzembe au kulikuwa na mpango wa kutengeneza mianya ya rushwa, kwa baadhi ya watumishi wasio waaminifu kuchukua pesa za waliofika hapo na kuwaingiza kinyemela, badala yake watu wakazidi kuwa wengi na kuleta mtafaruku wakati wa kuingia uwanjani.

Pili ni kwamba kumekuwa na utamaduni wa ajabu kidogo Uwanja wa Benjamin Mkapa wa kufungua baadhi ya mageti na mengine hayafunguliwi. Hii inasababisha msongamano mkubwa usio wa lazima na kusababisha kero na usumbufu kwa mashabiki.

Uwanja ule una milango mingi ambayo ikitumiwa vizuri sidhani kama kungetokea vurugu au mtafuruku wowote kwa mashabiki na walinzi wa uwanja huo pamoja na vyombo vyetu vya usalama.

Kulikuwa na dhana hapo awali kuwa mashabiki wengi wa 'Kibongo' kuja uwanjani kwa wakati mmoja, hivyo kusababisha msongamano, lakini jambo hili kwa sasa halipo.

Mashabiki wengi wameanza kuelimika kwani hawanunui tena tiketi kwenye magari uwanjani, wanazipata kwenye simu zao na madukani, kwa maana hiyo kila mmoja anafika kwa muda wake, wapo wakaoingia hata saa nne asubuhi.

Ushauri wa bure kwa Jeshi la Polisi, wakati mwingine kwenye mkusanyiko wa watu kama katika viwanja vya soka ni muhimu zaidi kutumia busara kuliko nguvu na tatizo ni kwamba nguvu hutumika pale hali imeshakuwa mbaya, hivyo kuwa mbaya zaidi.

Jambo lingine ni kuwa imefika wakati sasa milango yote ya Uwanja wa Benjamin Mkapa iwe inafunguliwa hasa kwenye mechi kubwa ili kuzuia msongamano mkubwa wa watu.

Huwa tunaona hata mechi ikiisha, badala ya milango na mageti kuwa wazi ili watu watoke kwa uhuru na amani, linaweza kufunguliwa geti upande mmoja na mlango mmoja, hivyo usalama wa watazamaji na mali zao kuwa mashakani.

## HABARI KITAIFA

# CCM yashtuka VVU/UKIMWI kuonekana kitu cha kawaida

**Na Nebart Msokwa,**
MUFINDI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimekemea tabia ya wananchi wa Mkoa wa Iringa kuona VVU/UKIMWI ni jambo la kawaida na hivyo kutojikinga.

Kimesema hali inayosababisha mkoa huo kuendelea kuwa na kiwango cha juu cha maambukizi huku idadi kubwa ya watoto wakibaki yatima.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Sophia Mjema, alikemea tabia hiyo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika mjini Mafinga wilayani Mufindi. Alifuatana na Katibu Mkuu wa chama hicho, Daniel Chongolo.

Alisema tatizo hilo siyo la kawaida kama ambavyo wananchi wa mkoa huo wanachukulia na hivyo akawataka kuhakikisha wanajikinga ili kupunguza kiwango cha maambukizi. Alisema moja ya sababu ya maambukizi katika mkoa huo kuwa juu ni ulevi wa kupindukia wa pombe za kienyeji aina ya ulanzi. Wakishalewa huwa hawakumbuki kutumia kinga wakati wa kujamiiana.

Sophia alisema watoto wengi wanaobaki yatima baada ya wazazi wao kufariki dunia huwa wanageuka kuwa vibaka na watoto wa mitaani, jambo ambalo linasababisha matukio ya uhalifu kuendelea kushamiri katika jamii. "Hili siyo jambo la kawaida. Ni janga kubwa sana ndugu zangu wengi mkilewa ulanzi mnajisahau na kujiachia. Jambo hili linasababisha VVU kuendelea kuenea. Unapofanya vitendo hivyo, ujue kwamba una watoto ambao watabaki yatima. Kwa hiyo, lazima ujikinge," alisema Mjema.

Alisema kwa sasa serikali inaboresha huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo elimu na afya na hivyo inahitaji wataalamu wengi wenye nguvu na afya lakini UKIMWI unaweza ukawa kikwazo cha kuharibu nguvu kazi ya taifa.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego, alisema mkoa huo unashikilia nafasi ya pili kitaifa kwa kuwa na maambukizi ya juu ya VVU. Siyo sifa nzuri kwa wananchi wa mkoa huo ambao wananchi wake wanafanya kazi kwa kujituma.

Alisema mpaka sasa kiwango cha maambukizi ni asilimia 11.3 na wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ili wajue madhara ya janga hilo na namna ya kujikinga wasiambukizwe.

Alisema kuwa na maambukizi ya juu ya VVVU ni moja ya mambo yanayochafua sifa ya mkoa huo na hivyo akawasisitiza wananchi kujilinda na kuwalinda wengine ili wasiambukizane.

"Tatizo lingine linalotukera ni udumavu. Mkoa wetu ni miongoni mwa mikoa inayozalisha chakula kwa wingi sana nchini lakini udumavu upo kwa kiwango kikubwa. Hii nayo siyo sifa nzuri kwetu," alisema Halima.

Katibu Mkuu wa CCM, Chongolo, aliwataka wananchi wa mkoa huo kutunza chakula wanachozalisha ili kuepuka kukumbwa na uhaba wa chakula baada ya kukiuza na hivyo kuendelea kukabiliwa na tatizo la udumavu. Alisema serikali inaendelea na mipango ya kuhakikisha mbolea inaendelea kuwafikia wakulima katika maeneo yao na kwa bei ya ruzuku ili kuongeza uzalishaji.

# Muhimbili kupandikiza figo kwa kutumia roboti

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH) inajipanga kuanza upandikizaji wa figo kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya matumizi ya roboti kama sehemu ya kuhamasisha utalii wa tiba.

Mwishoni mwa wiki, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Figo wa hospitali hiyo, Jonathani Mngumi, alibainisha hayo alipozungumza katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam.

Ni baada ya kurejea nchini akitoka India ambako yeye na madaktari bingwa 10 walikwenda kuangalia fursa za ushirikiano na hospitali za nchi hiyo katika kuimarisha utalii wa tiba nchini. Madaktari hao bingwa waliambatana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii Tiba, Abdulmalik Mollel ambaye ni Mkurugenziz wa Global Education Link na Global Medicare, akimwakilisha Mwenyekiti wake, Prof. Mohamed Janabi, Mkurugenzi Mkuu wa MNH. Dk. Mngumi alisema kwa muda wa siku 13 walizokuwa India, walitembelea hospitali mbalimbali kubwa za nchi hiyo ambazo zinatumia utaalamu wa hali ya juu katika utoaji wa huduma za matibabu.

Alisema kuwa ingawa na huduma za kibingwa zinazotolewa na MNH zinafanana na zile zinazotolewa India, kuna mambo mapya wamejifunza ambayo wanatarajia kuyatekeleza nchini kama sehemu ya kuvutia wagonjwa wa nje ya nchi kuja kutibiwa nchini.

"Tumeona wanavyomudu kupandikiza figo kwa kutumia roboti. Kwa hiyo huduma hizo zote tutahakikisha zinakuja hapa kwetu. Mpaka sasa tuko sehemu nzuri na tunaweza kuendelea na utalii tiba kwa kupokea wageni kutoka nje ya nchi kwa sababu huduma zetu ni za hali ya juu," alisema.

Dk. Mngumi alisema yeye na timu ya madaktari bingwa waliokwenda India watashauri mambo mazuri yote waliyoyaona huko ili yafanyike nchini kama sehemu ya kuimarisha utalii tiba kwa wageni kutoka nje.

Alisema MNH ina vifaa vya kisasa kama mashine za kuchuja damu kwa wagonjwa wa figo ambazo zinafanana na zile zinatumika India na wao wamekuwa wakipunguza gharama za matibabu kwa serikali kuchangia matibabu ya figo.

Daktari bingwa wa upasuaji wa moyo, mishipa na kifua kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Alex Joseph, alisema wamepata uzoefu namna wataalamu wa nchi hiyo wanavyotoa tiba ya upasuaji wa moyo.


**INVITATION FOR BIDS (IFB)**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

TAWA

**TANZANIA WILDLIFE AUTHORITY (TAWA)**

**Project: Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD)**

**(KfW Contract Reference No.:2012 66 451)**

**29th May 2023**

1. The Government of the United Republic of Tanzania has received a grant from the German State-Owned Investment and Development Bank (KfW) towards the costs of implementing the Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD), and intends to apply part of the proceeds towards payments under the contract for Construction of Rural Infrastructure (i.e., Socio-economic Infrastructures) in Selous Game Reserve (SGR).

2. The Tanzania Wildlife Authority (TAWA) now invites sealed bids from eligible and qualified bidders for the construction works comprised of various rural Socio-economic Infrastructures as shown in the table below:

| Package Number | Tender Number | Procurement Plan Number | Tender Description |
|---|---|---|---|
| 010 | MNRT/GOPA/KINGOFFICE&GUESTPP15 | PP 15 | Construction of an Office Block, Guest House and Water Tank Tower for Selous Game Reserve at Kingupira Sector Headquarter |
| 011 | MNRT/GOPA/KINGGARAGEPP16 | PP 16 | Construction of a Garage at the Selous Game Reserve at Kingupira Sector Headquarter |
| 012 | MNRT/GOPA/MIGURDORMPP17 | PP 17 | Construction of a Dormitory Building and Water Tank Tower for Selous Game Reserve at Miguruwe Sector Headquarters |
| 013 | MNRT/GOPA/LIWALEOFFICEPP18 | PP 18 | Construction of an Office Building and Water Tank Tower for Selous Game Reserve at Liwale Sector Headquarters |

***Note:***
- ***Bidders are allowed to submit offers for more than one package***
- ***All lots within a package must be included in the bid.***

3. Bidding will be conducted by means of the National Competitive Bidding (NCB) procedure with the qualification as specified in the KfW Guidelines for Procurement of Goods, Works and associated Services in Financial Cooperation with Partner Countries ("KfW Guidelines"

   **https://www.kfw-entwicklungsbank.de/PDF/Download-Center/PDF-Dokumente-Richtlinien/FZ-Vergaberichtlinien-V-2021-EN.pdf).**

4. A complete set of the bidding documents **(in English)** is available to interested eligible Bidders upon the submission of a written application to the address below and upon payment of a non-refundable fee of **Tanzanian Shillings One Hundred Thousand only (TZS 100,000.00).** The method of payment is via bank deposit to the following account at **Tanzania CRDB bank - Account name: Selous Ecosystem Conservation and Development with Account number 0150555174201.**

   The documents shall be sent by Courier (related costs to be covered by the interested Bidder) or physical pickup by the Bidders at ***Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.***

5. Bids in one original plus two paper copies and one digital copy, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below: **SECAD Project Manager, Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania** on or before **Monday 3rd July 2023 at 12:00 hours EAT**. Electronic bidding will not be permitted and late bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the bidders' or designated representatives and anyone who choose to attend at the address below on **Monday 3rd July 2023 at 14:00 hours at MNRT Room No. L406.**

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT)**
**c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No.L406, PO Box 25295,**
**40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Contact: - SECAD Project Coordinator**
**Email: - SECADtenders@gopa-infra.de**



**INVITATION FOR BIDS (IFB)**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

TAWA

**TANZANIA WILDLIFE AUTHORITY (TAWA)**

**Project: Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD)**

**(KfW Contract Reference No.:2012 66 451)**

**29th May 2023**

1. The Government of the United Republic of Tanzania has received a grant from the German State-Owned Investment and Development Bank (KfW) towards the costs of implementing the Selous Ecosystem Conservation and Development Programme (SECAD), and intends to apply part of the proceeds towards payments under the contract for Construction of Rural Infrastructure (i.e., Socio-economic Infrastructures) in Selous Game Reserve (SGR).

2. The Tanzania Wildlife Authority (TAWA) now invites sealed bids from eligible and qualified bidders for the construction works comprised of various rural Socio-economic Infrastructures as shown in the table below:

| Package Number | Tender Number | Procurement Plan Number | Tender Description |
|---|---|---|---|
| 014 | MNRT/GOPA/ KINGUPIRALOT1PP09 | PP 09 | Construction of Drainage Structures for Selous Game Reserve at Kingupira Sector |
| 015 | MNRT/GOPA/LIWALE LOT2PP10 | PP 10 | Construction of Drainage Structures for Selous Game Reserve at Liwale Sector |

***Note:***
- ***Bidders are allowed to submit offers for more than one package***

3. Bidding will be conducted by means of the National Competitive Bidding (NCB) procedure with the qualification as specified in the KfW Guidelines for Procurement of Goods, Works and associated Services in Financial Cooperation with Partner Countries **("KfW Guidelines" https://www.kfw-entwicklungsbank.de/PDF/Download-Center/PDF-Dokumente-Richtlinien/FZ-Vergaberichtlinien-V-2021-EN.pdf).**

4. A complete set of the bidding documents **(in English)** is available to interested eligible Bidders upon the submission of a written application to the address below and upon payment of a non-refundable fee of **Tanzanian Shillings One Hundred Thousand only (TZS 100,000.00).** The method of payment is via bank deposit to the following account at **Tanzania CRDB bank - Account name: Selous Ecosystem Conservation and Development with Account number 0150555174201.**

   The documents shall be sent by Courier (related costs to be covered by the interested Bidder) or physical pickup by the Bidders at ***Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.***

5. Bids in one original plus two paper copies and one digital copy, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below: **SECAD Project Manager, Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT), c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No. L406, PO Box 25295, 40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania** on or before **Friday 7th July 2023 at 12:00 hours EAT.** Electronic bidding will not be permitted and late bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the bidders' or designated representatives and anyone who choose to attend at the address below on **Friday 7th July 2023 at 14:30 hours at MNRT Room No. L406.**

**Ministry of Natural Resources and Tourism (MNRT)**
**c/o GOPA, Mpingo House, 4th Floor, Room No.L406, PO Box 25295,**
**40 Julius Nyerere Road, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Contact: - SECAD Project Coordinator**

# Samia atoa ndege kusafirisha mwili wa Mkono, kuzikwa leo

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa usafiri wa ndege kwa ajili ya kuusafirisha mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Butiama (CCM), Nimrod Mkono (79) kutoka Dar es Salaam kwenda Kijiji cha Kigori Busengwe mkoani Mara. Mwili wa Mkono uliwasili juzi alfajiri katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) ukitokea Marekani kisha kupelekwa nyumbani kwake Masaki.

Mkono aliyekuwa akitibiwa tangu mwaka 2018 huko Marekani, alifariki dunia Aprili 18 mwaka huu.

Akizungumza wakati wa ibada ya kuaga mwili nyumbani kwake, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Mazishi, Stephen Wasira, alisema Rais Samia ametoa ndege hiyo kutokana na mchango wa Mkono alioutoa serikalini enzi za uhai wake. "Mbali na heshima hiyo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alimwakilisha Rais Samia leo katika kuaga mwili wa Mkono katika Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam," alisema. Wasira alisema kuwa baada ya mwili huo kuagwa kitaifa, utasafirishwa kwa ndege hiyo na mazishi yatafanyika Butiama Mei 29, yaani leo.

Aliyekuwa Mbunge wa Musoma Mjini 2010-2015 (CHADEMA), Vincent Nyerere, alisema mkono alikuwa mtoaji mzuri wa misaada mbalimbali ya kimaendeleo jimboni bila kuangalia tofauti za kiitikadi.

Alisema kila alipokuwa anapata tatizo la kisheria ama tafsiri ya miswada bungeni, Mkono alikuwa anamsaidia kwa kumpa ufafanuzi. Vincent alitolea mfano miundombinu ya Musoma ilikuwa na tatizo lakini Mkono alimsaidia namna ya kuishauri serikali kuhamisha miradi ya barabara kutoka halmashauri hadi Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) bila kukiuka sheria.

"Mkono alipenda sana elimu, alisisitiza watu wa Mara kusoma, muda mwingi alitumikia wananchi kuliko hata familia yake, tena kwa rasilimali zake mwenyewe bila kudai," alisema.

Mkono alikuwa Mbunge wa Musoma Vijijini mwaka 2005 hadi 2015 na baadaye Mbunge wa Butiama mwaka 2015 hadi 2020 kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Enzi za uhai wake, alichangia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kujenga shule za msingi na sekondari za Chiefu Ihunyo, Chiefu Wazangi, Oswald Mang'ombe, Shule ya Sekondari Butuguri na ile ya Kasoma kisha kuzikabidhi serikalini.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (katikati), akipata maelezo ya huduma zinazotolewa na Bank of Africa Tanzania kutoka kwa Meneja wa kitengo cha utoaji fedha za biashara, Jesca Mizamba (kushoto), alipotembelea banda la maonyesho la benki hiyo kwenye mkutano wa mwaka wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi uliomalizika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Misaada kwa yatima kutolewa kwa usawa

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema serikali inaratibu mpango wa kitaifa wa kupokea na kutoa misaada katika vituo vya kulelea yatima kwa usawa.

Amesema lengo ni kuvifikia vituo vyote na kutoa misaada kwa uwiano badala ya kunufaika vichache vinavyofikiwa na wadau wakati vingine vikikosa misaada.

Waziri huyo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipomwakilisha Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Hussein Mwinyi, kupokea msaada wa watoto yatima kwa Kituo cha Ijango Zaidia kutoka kwa Mke wa Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Prof. Peng Liyuan.

Msaada huo ni utekelezaji wa mpango wa kusaidia watoto yatima unaofahamika kwa jina la 'Gusa Moyo Watoto' ulioanzishwa na Mke wa Rais wa China na kushirikisha wake wa marais wa nchi nyingine duniani kwa lengo la kuhakikisha watoto hao wanakuwa na maisha bora.

"Wote wanaotakiwa kusaidia watoto wapite njia moja, tuwe na mfuko wa pamoja wa kupokea misaada yote ili kuunganishwa na bajeti ya wizara yetu kwa ajili ya kusambaza katika vituo vyote ili kutimiza malengo ya wake wa marais hawa kutoa misaada hii kwa walengwa wote," alisema.

Dk. Dorothy alisema wataratibu wadau wote wenye nia ya kusaidia watoto yatima ili kufikia walengwa na kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufikia malengo waliyojiwekea ya kugusa watoto wa Tanzania.

Akisoma risala ya Mama Mariam Mwinyi, waziri huyo alinukuu, "Ninashukuru taasisi zote za serikali na watu binafsi kwa kuendelea kujitoa na kusaidia watoto walio katika mazingira magumu ili kufikia kundi kubwa la wasiyojiweza."

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, alisema wametoa misaada ya maziwa, vifaa vya michezo, dawa na vifaa vya shule kama madaftari na kalamu kwa ajili ya kituo hicho.

Alisema ushirikiano uliopo baina ya nchi hizo mbili umesukuma kutekelezwa kwa mpango huo nchini na mke wa Rais wa China, Prof. Peng wenye lengo kusaidia watoto yatima katika kuadhimisha Siku ya Mtoto.

"Kwa ushirikiano tulionao baina ya nchi hizi mbili, tunajali wanawake na watoto wa Tanzania hasa waliopo katika mazingira magumu na tayari tumeshatoa misaada mingine mingi ikiwamo kompyuta, redio, baiskeli, masweta, mablangeti na vifaa vya shule kwa wanafunzi katika kusaidia wanawake na watoto wa Tanzania kuishi maisha mazuri wanayotarajia," alisema Balozi Mingjian.

# Wabunge wasifu utekelezaji mradi wa bomba la mafuta

**Na Denis Fusi**

WABUNGE wamesifu mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP) kwa kutoa fidia nzuri kwa waliopitiwa na mradi huo na kutoa kipaumbele katika maeneo mengine ikiwamo utunzaji wa mazingira.

Pia wamepongeza uamuzi wa kuwapa mafunzo ya kilimo, ufugaji na elimu kuhusu matumizi ya rasilimali fedha walizolipwa fidia wananchi waliopitiwa na mradi huo.

Wakizungumza wakati wa semina iliyoandaliwa na EACOP kwa ajili ya kutoa mrejesho wa hatua iliyofikiwa na mradi huo mpaka sasa kwa wabunge, watunga sheria hao, akiwamo Japhet Hasunga wa Jimbo la Vwawa mkoani Songwe, walisema tofauti na propaganda zinazoenezwa, mradi huo upo tofauti sana na miradi mingine.

Hasunga alisema kuwa kwa kiasi kikubwa unazingatia sheria za nchi na zile za kimataifa katika utekelezaji wake.

"Tumeona kwa kiasi gani watu wamejengewa nyumba nzuri tofauti na zile walizokuwa wanamiliki hapo awali kabla ya kufikiwa na mradi.

"Pia wamepewa chakula cha kukidhi mahitaji ya familia zao kwa kipindi cha mwaka mzima na mafunzo mbalimbali juu ya kilimo bora cha kisasa na ufugaji," alisema Hasunga.

Mbunge Selemani Zedi wa Jimbo la Bukene mkoani Tabora, alisema ni shuhuda wa yaliyofanywa na mradi huo kwa wananchi wake waliopitiwa na mradi huo.

"Mradi umechukua zaidi ya ekari 400 za wananchi wangu, ambao wamepewa nyumba nzuri zilizobadilisha maisha yao ikiwa kama sehemu ya fidia.

Hao wanaosema mradi huu hauzingatii haki za binadamu, waje waone na wanaosambaza propaganda hizi kwa sisi tulioguswa na mradi tunawashangaa kiukweli," alisema Zedi.

Mbunge Esther Bulaya wa Viti Maalum alisema serikali inatakiwa kuhakikisha kilichofanywa na mradi wa EACOP pia kinafanyika katika utekelezaji wa miradi mingine kwa kuwapa nafuu ya maisha wale wanaoguswa.

"Kuna vitu kama taifa tunaweza kujifunza katika ulipaji fidia kupitia mradi huu wa EACOP, ikiwamo juu ya ushirikishwaji wa wananchi wanaoguswa ambapo wanapaswa kuridhika na faida wanazopewa.

"Miradi inapokuja isilete umaskini, bali watu wafurahie miradi hiyo na tumejifunza katika mradi wa EACOP, watu wamepewa nafasi ya kuchagua fidia ya nyumba au fedha na kunufaika na programu nyingine ikiwamo kupewa mbegu kwa ajili ya kilimo," alisema Bulaya.

Akizungumza kwa niaba ya serikali, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema serikali imeridhika na hatua zilizofikiwa mpaka sasa, ikiwamo suala la watu kulipwa fidia, utunzaji wa mazingira na maandalizi kiujumla ya mradi huo.

"Tunaendelea kusimamia kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa ili kuiletea nchi maendeleo kupitia mradi huu ikiwamo kunufaika na kodi mbalimbali zinazopatikana," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa EACOP, Martin Tiffen alisema kikao hicho cha ushirikishwaji kwa wabunge kilijumuisha awamu tatu zilizohusu maeneo muhimu ya mradi, ikiwa ni pamoja na watoa huduma wa ndani, ardhi na masuala yanayohusu jamii na mazingira.

Alisema lengo la kukutana na wabunge ni kuwapa mrejesho wa kilichofanyika na kinachokwenda kufanyika.

Mwakilishi wa mradi huo kwa upande wa serikali kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Asiadi Mrutu, alisema sehemu kubwa ya fidia imeshalipwa. Wananchi wanajiandaa kuondoka katika maeneo ya mradi kwa ajili ya kuanza rasmi ujenzi.

Mkuu wa Kitengo cha Kujenga Uwezo kwa Watoa Huduma wa Ndani katika Kampuni ya EACOP, Martha Makoi, alitoa maelezo muhimu kuhusu watoa huduma wa ndani na kujenga uwezo, akisisitiza kuwapo ushirikiano baina ya EACOP na Bunge.



# Utouh avipa mtihani vyuo vikuu utafiti wa ajira

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (mstaafu), CAG-Ludovick Utouh, amevipa mtihani vyuo vikuu nchini, kujitosa kufanya utafiti wa kina wa aina gani ya mahitaji ya ajira za watumishi wa umma wanaotakiwa kwa sasa ili kuipunguzia serikali mzigo wa watumishi kutokana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

Utouh ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, aliwapa kibarua hicho wanazuoni wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) mwishoni mwa wiki, kabla ya kuzindua kamati ya ushauri wa mahusiano na sekta binafsi/soko la ajira, iliyopewa jukumu la kushauri katika mradi wa kitaifa wa elimu ya juu wa mageuzi ya kiuchumi (HEET).

Kamati hiyo ya wanazuoni, inaundwa na Mkuu wa Tume ya TEHAMA nchini, Dk. Mkundwe Mwasaga, Msajili wa zamani wa Hazina, Dk. Oswald Mashindano, Agapiti Manday, Anthony Chamanga, Prof. Fedy Kilima, CPA (T) Josephat Kisamalala, Laurine Kilemwa, Godfrey Ng'urah na Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Akiba na Mikopo (SCCULT), Hassan Mnyone.

"Mimi nilipokuwa CAG, nikifanya ukaguzi wa ikama serikalini, na iko mpaka leo, kuna local government (serikali za mitaa), unaletewa ina shortage ya manpower (upungufu wa watumishi). Is that true? ni kweli kwamba hiyo shortage ipo?

"Ningelishukuru sana kama vyuo vyetu vikuu, vingejitoa vikafanyia utafiti wa kina the manpower requirement ya serikali yetu (mahitahi ya ajira) ili vitatue huo utata ni watumishi wa aina gani jumla.

"Serikali inakwenda kwa ikama zilizoandikiwa katika miaka iliyopita, lakini mambo yamebadilika. Sasa huhitaji kuwa na secretary (mhazili), wewe unaona hesabu yako ukiwa ofisa kuwe na secretary, wakati kila kitu unakiona kwenye system (mfumo) na unaweza ukafanya mwenyewe."

Kuhusu mchakato wa kuifumua mitaala na kukuandaa programu mpya zitakazoamua hatima ya wanaohitimu elimu ya juu kukabiliana na soko la ajira, Utouh, alikipongeza Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kuonyesha nia ya dhati ya kutaka mabadiliko katika mfumo wetu wa elimu.

"Mitaala iliyopitwa na wakati, mafunzo yaliyopitwa na wakati, na njia za ufundishaji zilizopitwa na wakati, huwaacha wanafunzi bila ya kuwa na ujuzi wa kukabiliana na mabadiliko yanayotokea kwa haraka duniani.

"Ni kweli taifa lolote ambalo halifanyi maboresho katika mfumo wake wa elimu, kuna hatarisha kuachwa nyuma kimaendeleo. Kwa hiyo, juhudi za pamoja zinahitajika ili kufikia lengo namba nne la malengo endelevu ya elimu la Umoja wa Mataifa," alisisitiza Utouh.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi wa HEET, Mratibu wa mradi huo kutoka MoCU, Prof. Fredy Kilima, ambaye ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mipango, Fedha na Utawala, alisema mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/2026) na unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia mkopo wa Benki ya Dunia, chuo hicho kimepatiwa Shilingi bilioni moja.

Alisema kupitia mradi huo, chuo kimelenga kuboresha mambo mbalimbali ikiwamo kuboresha mazingira ya kujifunzia na ufundishaji, kwa kujenga majengo mapya, kufanya marejeo ya mitaala mipya yenye kuleta tija katika soko la ajira, kuwajengea uwezo wanazuoni kuwa wabunifu na kumudu kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano na kuhamasisha matumizi ya teknolojia.

# Wanasiasa waonywa kuingilia shughuli za kitaaluma

**Na Hamida Kamchalla,** MKINGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, amewaonya wanasiasa mkoani humo kuacha kuingilia masuala ya taaluma, hasa yanayohusiana na kada ya uuguzi, kwa kuwa wanawavuruga na kuwaondoa kwenye ari ya kutekeleza majukumu yao kwa weledi na uadilifu.

Kindamba, aliwanyooshea kidole wanasiasa hao mwishoni mwa wiki, wakati alipokutana na wauguzi katika Wilaya ya Mkinga, alikokwenda kusikiliza na kutatua kero zao.

"Hakuna kiongozi yeyote wa siasa kuanzia sasa, ataigusa sekta ya afya nikiwapo Tanga. Mambo yao yatamalizwa na bodi yao, kwa kuwa ipo na inasimamia masuala yao, kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma.

"Onyo hili nalitoa kwa wanasiasa, si Mwenyekiti wa Chama, Diwani, wala Mbunge hamruhusiwi kwenda kuingilia kazi za uuguzi. Hili ni marufuku katika Mkoa wa Tanga; taaluma hii ina vyama na bodi zao, acheni mambo ya wauguzi yamalizwe na vyombo vyao vinavyowasimamia."

Aliwageukia pia wauguzi akiwataka kufanya kazi zao kwa weledi, kwa kuwapokea na kuwahudumia vizuri wagonjwa ili kuepuka malalamiko ya wananchi.

"Wauguzi, muwe na sifa nzuri ya upokeaji na utaoaji huduma bora na kwa weledi. Najua siyo wote, lakini wapo wanaolalamikiwa, nendeni mkajitathmini," alisisitiza mkuu huyo wa mkoa.

Awali, katika kikao kazi hicho, Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi, Mkoa wa Tanga, Abeid Njopa, aliiomba serikali kuingilia kati suala la wanasiasa wanaowadhalilisha na kuwatolea maneno ya kashfa wauguzi wanapokuwa wakitimiza majukumu yao.

Njopa, alimweleza Kindamba kwamba mkoa huo, una upungufu wa wauguzi ikilinganishwa na wingi wa wagonjwa, kwa sasa wako wauguzi 1,267 sawa na asilimia 39.3, wakati upungufu ni 2,024 sawa na asilimia 60.7. Kwa mujibu wa Njopa, mahitaji ni wauguzi 3,224.


EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

## MAOMBI YA KUONESHA NIA YA UTOAJI WA HUDUMA ZA UKARABATI KATIKA JENGO LA OFISI ZA MAKAO MAKUU YA EACOP KUMBUKUMBU NA. 00000234

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, ("EACOP LTD") inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa huduma za ukarabati katika jengo la ofisi za makao makuu ya Mradi wa EACOP

Mradi wa EACOP unajumuisha shughuli za ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani, karibu na Mkoa waTanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU HUDUMA**

Kampuni EACOP Ltd, inatumia sehemu ya ghorofa nne zenye jumla ya mita za mraba [***] katika Jengo lililopo Kitalu 1, Kiwanja Na. 1403 nyumba Na. 7, Mtaa wa Bains Avenue, Off Chole, Dar es Salaam. Kama sehemu ya matengenezo na utunzaji wa maeneo yanayotumiwa na ofisi zake, Kampuni ya EACOP Ltd inahitaji huduma ya mtu/makampuni yenye sifa kutoa huduma zifuatazo;

- Kufanya ukarabati na/ama wa mara kwa mara au wa kulinda mfumo wa HVAC.
- Kufanya ukarabati na/ama wa mara kwa mara au wa kulinda mifumo ya maji ya jengo,(ikiwa ni pamoja na kubadilisha machujio, vifuniko, gasiketi, n.k)
- Kufanya ukarabati na /ama wa mara kwa mara au wa kulinda seti ya mfumo wa jenereta kwenye jengo ikiwa ni pamoja na (ATS, elementi za chujio, Kubadilisha Mafuta nk)
- Kupigiwa simu kwa ajili ya usaidizi wa kazi za matengenezo ya dharula (Kazi za Umeme, Mfumo wa Usafi (ikujumuisha matengenezo ya mabomba yanayohusiana na pampu ya jengo, kudhibiti uvujaji kutoka kwenye mabomba na valvu, Miundo mbinu ya usafi, miundo mbinu ya usambazaji wa maji n.k), Mifumo ya AC (kama ipo ).
- Kupigiwa simu kwa jili ya Kazi za matengenezo madogo / ya kati ya (Mitambo / Umeme).
- Kuzibua mambomba ya mifumo ya maji na maji taka, maunganio ya mabomba na vifuniko vya kalo. Usambazaji wa maji, Mashimo ya maji taka & kazi ya Uteketezaji Maji taka

  **Kumbuka:** Orodha ni kielelezo tu na sio kamili kabisa. Wigo wa kazi na huduma utakamilishwa baada ya EOI na utajumuishwa katika CFT itakayotolewa baadae.

**VIGEZO MUHIMU:**


**Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo.**

- Cheti halali cha kampuni na leseni ya biashara
- Cheti cha namba ya utambuzisho wa mlipa kodi pamoja na cheti cha TRA cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili au wametuma maombi ya kujisajili kwenye kazi data ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Usajili wa mamlaka husika wa hivi karibuni ikijumuisha OSHA, CRB, etc
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017
- Uzoefu wa awali wa kutoa Huduma zinazofanana na huduma za Ukarabati kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita.
- Provide proof of financial capacity and financial statement for the previous financial year
- Uthibitisho uwezo wa kifedha na taarifa ya kifedha ya mwaka wa fedha uliopita
- Upatikanaji wa rasilimali za Kiufundi (Lazima kuambatanisha na sifa bainifu (CV) na uzoefu wa miaka ya kutoa huduma
- Barua ya uthibitisho kuhusu usimamizi wa miundo mbinu na ukarabati wa vitu katika mawanda unganifu yanajuumuisha Ukarabati na Matengenezo ya Ofisi kutoka kwa miradi iliyotekelezwa hapo awali katika kipindi cha miaka 5 iliyopita kama vile miradi ya (Bomba, Umeme, Ukarabati wa vyoyozi, Ufundi seremala, Upakaji rangi, Ufundi washi).

Makampuni yenye uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu yanakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**). Maombi yatumwe mnamo au kabla ya tarehe **11 Juni 2023 saa 11 jioni** saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **00000234 - Utoaji wa huduma ya Matengenezo na Ukarabati Mkubwa katika Mradi wa EACOP**

Maombi yote ya kuonesha nia (EOI) yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.





# Kanda ya Ziwa kunufaika mtandao wa satelaiti

**Na Neema Emmanuel,**

MWANZA

WANANCHI kutoka katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, wanatarajiwa kunufaika na huduma ya mtandao wa satelaiti yenye kasi zaidi kwa gharama nafuu itakayo wasaidia katika kufanikisha shughuli zao mbalimbali hususani za kimtandao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo jijini Mwanza, Ofisa mauzo wa Konnect Broadband Tanzania, Obafemi Agbanrin, alisema imani yao ni kuwa kila mtu anapaswa kuwa na intaneti yenye ubora na kasi ya hali ya juu popote alipo na huduma hiyo ili kuwapa watu kufikia fursa ya kibinafsi na za kitaaluma.

"Ni kampuni mpya inayokupa ya mtandao wa satelaiti yenye kasi zaidi iliyopo chini ya kampuni mama iitwayo Eutelsat mojawapo ya waendeshaji wakubwa zaidi duniani wa satelaiti na hatua hii ni baada ya kuona hali ya kusuasua kwa mtandao katika maeneo ya visiwani na vijijini hivyo kumaliza tatizo hilo," alisema.

Akieleza vifurushi vya mtandao huo, Ofisa masoko wa Fanix Africa, Paul Ammassy "Kwa wale wenye uwezo wa kununua dishi vifurushi vyao vinaanzia 60,000 kwa matumizi binafsi vinaanzia Sh. 300 kwa siku hadi 18,000 kwa mwezi hiyo yote tunalenga kuwafikia watu wote kinachotakiwa ni kuwa na simu njanja na application ya connect wi-fi huduma ya vocha ambazo siyo za kikwangua itatolewa na wakala ambao watasambaa kila mahali," alisema.

# MaDC wacharuka utendaji mbovu watumishi

**Na Waandishi Wetu**

WAKUU wa wilaya Bukoba na Shinyanga wamekerwa na utendaji kazi mbovu wa baadhi ya watumishi wa manispaa na wilaya hizo kwa ujumla hali inayokwamisha shughuli za kimaendeleo katika maeneo yao na kushindwa kufikia malengo katika mikakati wanayojiwekea kila mwaka.

Wakuu hao wa wilaya wametema nyongo zao kwa nyakati tofauti, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Erasto Sima, akizungumza mwishoni mwa wiki katika kikao cha Baraza la Madiwani Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, alisema licha ya serikali kutoa fedha nyingi katika manispaa hiyo mambo yamekuwa hayaendi ipasavyo kutokana na baadhi ya wataalamu kushindwa kutimiza majukumu yao.

"Mstahiki Meya naongea kwa masikitiko sana huna watendaji na wataalamu wachapa kazi katika halmashauri hii, mfano Agosti 9, mwaka huu, tunatarajia kupokea Mwenge wa Uhuru ukitoka wilayani Muleba, lakini mpaka sasa miradi inasuasua wataalamu wameshindwa kuchambua miradi na walipoagizwa kufanya hivyo wameleta tu miradi ya Sh. milioni 200 pekee katika halmashauri kubwa hivi mpaka kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya tunakaa kufanya kazi hiyo," alisema Sima.

Kuhusu ukarabati wa kituo cha mabasi cha Bukoba, Mkuu wa wilaya alisema ukarabati wa kituo hicho haufanyiki kikamilifu licha ya mabasi kuingia na kutoka kila uchwao na kulipia kodi hali inayoleta adha kwa wasafiri, wasafirishaji pamoja na wafanyabiashara wa eneo hilo.

"Mvua zikinyesha eti watu wanakanyaga matope katika mji hii aibu nyie hamuwezi kuiona? Madiwani, Mstahiki Meya pamoja na Mkurugenzi wa hakikisheni mnatimiza wajibu wenu hiyo stendi ifanyiwe marekebisho ya kudumu maana hata kituo cha mabasi kikikamilika hii itaendelea kutumika kama kituo cha daladala," alisisitiza Sima.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Johari Samizi, akizungumza katika mkutano mkuu wa nusu mwaka wa wadau wa maji kutoka Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA), Wilaya ya Shinyanga, aliwataka viongozi wote katika wilaya hiyo kufanya kazi kwa ushirikiano na siyo kujitokeza baadhi kukwamisha shughuli za maendeleo.

"Nawapongeza RUWASA Wilaya ya Shinyanga kuandaa mkutano huu wa kukutana na wadau wa maji ili kujadili mustakabali wa maendeleo ya huduma ya maji vijijini, nitumie pia fursa hii kuwasihi viongozi wote katika maeneo yetu kushirikiana kufanya kazi kwa pamoja na si kukwamisha shughuli za kimaendeleo," alisema Johari. Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Ngassa Mboje, alisema kwa sasa wilaya hiyo wananchi wake asilimia kubwa wanapata huduma ya majisafi na salama, na kuwataka RUWASA waendelee kutekeleza miradi ya maji kwa katika vijiji ambavyo vimesalia.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) Wilaya ya Shinyanga, Mhandisi Emmanuel Nkopi, alisema hali ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi wilayani humo ni asilimia 72.3, kwamba jumla ya wananchi 338,962 wanapata maji kati ya 468,611.




Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye (wa pili kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 165 kwa mjasiriamali Paulina Shao (wa pili kushoto) ambaye ni mwanzilishi mwenza wa kampuni ya B&L Agri Digital Ltd. Mkopo huo umetolewa na Benki ya Azania chini ya mpango wa SANVN-Viwanda unaoshirikisha Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), VETA, SIDO na NSSF, mkoani Kigoma mwishoni mwa wiki hii. Wengine ni Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa (wa tatu kulia), Meneja wa Benki ya Azania tawi la Geita, Rhoda Baluhya na viongozi wengine wa serikali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliokimbilia mgodini kukwepa masomo warejeshwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Sekondari Nyikoboko Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga waliokuwa wamesitisha masomo yao na kukimbilia migodi kufanya shughuli za uchimbaji madini wamerejeshwa shuleni baada ya kushauriwa na kuridhia kurudi.

Wakizungumza na Nipashe juzi baada ya mdahalo wa kupinga ukatili wa kijinsia uliondaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), wanafunzi hao walieleza walifanikiwa kurejeshwa kutoka katika machimbo hayo baada ya ushauri waliopewa na moja ya klabu ya wanafunzi kuhusu manufaa ya elimu kwa maisha ya baadaye.

Kule tulikuwa tukifanya kazi hatarishi hususani za kuingia katika miamba kutafuta madini pamoja na kuchota maji ya kuoshea dhahabu ambayo sio salama kwetu wenye umri mdogo," alisema Jackson Amosi mmoja wa wanafunzi hao.

Mwalimu wa malezi katika shule hiyo, John Banda alisema, wameanzisha dawati la malezi, unasihi, ulinzi na usalama kwa wanafunzi, litakalokuwa na dhima ya kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili ndani ya eneo la shule na kwenye jamii na kuzitatua ili wasikimbie masomo na kushindwa kutimiza ndoto zao.

Mwezeshaji kutoka TGNP, Jackson Malangalila, alisema, midahalo waliyoianzisha shuleni na ndani ya jamii imeanza kuleta matokeo chanya baada ya makundi mbalimbali kwenye jamii kutambua athari za ukatili wa kijinsia na kuanza kutafuta suluhisho ya kuzitatua kwa kutoa taarifa katika vyombo vya sheria ikiwamo ofisi ya mtendaji wa kata.

Nipashe
# Spotika



WACHEZAJI WA 5 WALIOPASWA KUWEPO TUZO YA EPL 2023 UK. 12-13



# MAKOCHA 5 WALIOKUMBWA NA RUNGU LA FA ENGLAND

POCHETTINO

## ISIKUPITE

KOCHA Jose Mourinho amesema Tottenham ndio klabu pekee aliyowahi kuifundisha lakini hakuwa na uhusiano nayo mzuri.
Mreno huyo anayefundisha Roma kwa sasa alifukuzwa kazi Tottenham Aprili 2021 baada ya kudumu kwenye klabu hiyo kwa miezi 17 tu.
"Natumaini mashabiki wa Tottenham hawatachukulia hii vibaya lakini ukweli ni kwamba katika klabu zote nilizowahi kufundisha, sikuwa na mapenzi ya 'ndani' na Tottenhma," alisema Mourinho.



**LONDON,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alitumikia adhabu ya kufungiwa mchezo mmoja ambao ulikuwa wa mwisho kucheza nyumbani msimu huu dhidi ya Aston Villa Jumamosi iliyopita, kwa kumkosoa hadharani mwamuzi, Paul Tierney baada ya Wekundu hao kuwalaza Tottenham Hotspur 4-3 kwenye Ligi Kuu mwezi uliopita.

Atafungiwa kwa mchezo wa pili iwapo atafanya ukiukwaji wowote zaidi kati ya sasa na mwisho wa msimu ujao.

Klopp alimbwatukia Tierney kuwa ana historia mbaya na Liverpool, baada ya kuoneshwa kadi ya njano kwa kusherehekea mbele ya ofisa wa nne, John Brooks baada ya bao la ushindi la dakika ya mwisho la Diogo Jota katika mchezo dhidi ya Aston Villa, Machi.

"Tuna historia yetu na Tierney, sijui ana nini dhidi yetu," alisema Klopp akiiambia Sky Sports.

"Amesema (hakuna) matatizo lakini hiyo haiwezi kuwa kweli. Jinsi anavyonitazama, sielewi. Huku Uingereza hakuna mtu anayepaswa kufafanua hali hizi, ni ngumu sana kuelewa. Alichoniambia aliponipa kadi ya njano si sawa."

Pep Guardiola aliepuka kufungiwa kutokana na matamshi aliyotoa kuhusu mwamuzi kabla ya mechi ya dabi ya Manchester mwaka 2018, lakini Klopp hayuko peke yake linapokuja suala la makocha wa Ligi Kuu England kufungiwa kwa mambo wanayosemwa kuhusu waamuzi.

**5. Jose Mourinho - mchezo 1 (2016)**

Jose Mourinho alifungiwa mchezo mmoja Novemba 2016 wakati wa msimu wake wa kwanza Manchester United, baada ya kumkabili Mark Clattenburg wakati wa mapumziko katika suluhu dhidi ya Burnley. Wakati huohuo, alipigwa faini ya pauni 50,000 kwa maoni aliyoyatoa kuhusu Anthony Taylor kabla ya pambano kati ya timu yake ya United na Liverpool.

Katika matukio mengine, Mourinho alipigwa faini ya pauni 10,000 wakati akiwa kocha wa Chelsea mwaka 2014 kwa maoni yake kuhusu Mike Dean baada ya kufungwa na Sunderland - msaidizi wake, Rui Faria aliishia kufungiwa michezo sita kwa kugombana na mwamuzi uwanjani baada ya mchezo huo huo.

Mwaka 2015, alitozwa faini ya pauni 50,000 na kufungiwa mchezo mmoja, baada ya kupendekeza kwamba Robert Madley 'aliogopa' kuipa Chelsea penalti katika kipigo cha nyumbani dhidi ya Southampton.

**4. Harry Redknapp - michezo 2 (2003)**

Katika kipindi chake kama kocha wa Portsmouth, Harry Redknapp alifungiwa mechi mbili baada ya kumkosoa mwamuzi Andy D'Urso na kuwasilisha malalamiko yake kwa ofisa wa nne, Lee Mason.

"Nilitilia shaka uchezeshaji wa mwamuzi, ambao nilifikiri haukufaa," alisema Redknapp. "Sikupiga kelele au kumtusi mwamuzi, nilitoa maoni kwa ofisa wa nne. Asilimia 99 ya maofisa wa nne wangesema 'Mimi nakubaliana na wewe' au 'Keti chini, Harry.' Nadhani alikuwa kijana ambaye labda alikuwa akijaribu kujipatia jina."

Mwaka 2010 akiwa Tottenham Hotspur, Redknapp alifanikiwa kukwepa kufungiwa, baada ya kutishia kuwa hatafanya tena mahojiano baada ya mechi, kwa maoni yaliyotolewa na mwamuzi, Mark Clattenberg.

**3. Mauricio Pochettino - michezo 2 (2019)**

Mike Dean alisema kuhusu kocha wa Tottenham Hotspur wa wakati huo, Mauricio Pochettino katika ripoti ya baada ya mechi mwaka 2019: "Hataacha kusema 'unajua ulivyo, unajua ulivyo'. Nilimwomba anieleze na akarudia 'unajua. wewe ni nini."

Mchezo huo ulikuwa wa kichapo cha Tottenham dhidi ya Burnley na Pochettino alijibu kwa hasira kwa kile alichoamini kuwa uamuzi usio sahihi wa kutoa kona ambayo ndio iliwafanya Burnley wapate ushindi.

**2. Arsene Wenger - michezo 3 (2018)**

"Wewe sio muungwana...wewe ni aibu," ni maneno ambayo yalitoka kinywani mwa Arsene Wenger kuelekea kwa mwamuzi Mike Dean baada ya mchezo wa Arsenal dhidi ya West Brom katika mkesha wa mwaka mpya 2017.

Mfaransa huyo alikasirishwa sana na mkwaju wa penalti wa dakika za lala salama uliotolewa kwa West Brom na baadaye aliingia kwenye chumba cha kubadilishia nguo ili kukabiliana na Dean.

Wenger alikosa mechi tatu mwanzoni mwa 2018 na alipigwa pia faini ya kulipa pauni 40,000.

**1. Sir Alex Ferguson - michezo 5 (2011)**

Kocha wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson aliishia kufungiwa michezo mitano kufuatia kumkosoa mwamuzi, Martin Atkinson baada ya kufungwa na Chelsea mwaka 2011.

"Unataka mwamuzi wa haki, au mwamuzi mwenye nguvu, hatukupata hilo. Lazima niseme, nilipoona mwamuzi ni nani niliogopa. Niliogopa sana," alisema Ferguson wakati huo na kusababisha FA kumfungia.

Raia huyo wa Scotland alifungiwa mechi tatu kwa matamshi hayo. Lakini sababu iliyomfanya aongezewe mechi mbili zaidi ni kwa sababu FA ilimpiga marufuku michezo miwili aliyosimamishwa tangu mwaka 2009 baada ya kuhoji hadharani utimamu wa mwili wa mwamuzi, Alan Wiley.

## Extra Time



DECLAN RICE

# WACHEZAJI WA 5 WALIOPASWA KUWEPO TUZO YA EPL 2023

**LONDON,** England

HUKU jana Jumapili ndio ulikuwa mwisho wa msimu wa Ligi Kuu England, ni wakati sasa wa kuwatambua wachezaji ambao wamesimamisha vichwa na mabega juu kwenye shindano hilo kwa kipindi cha miezi tisa iliyopita.

**Manchester City na Arsenal zimekuwa timu mbili bora za mgawanyiko huo, kwa hivyo labda haishangazi kwamba wana wachezaji wengi wanaowania tuzo rasmi za mwisho wa msimu za Ligi Kuu.**

Erling Haaland, Bukayo Saka na Martin Odegaard wameteuliwa kuwania tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi ya England na Mchezaji Bora Chipukizi wa Ligi hiyo.

Lakini hakuna ubishi kwamba, Haaland raia wa Norway na kila mchezaji mwingine aliyeteuliwa, wamekuwa na msimu bora zaidi kwao.

Lakini kuna baadhi ya wachezaji ambao wamepuuzwa ambao labda walistahili zaidi kwa sababu ya michango yao kibinafsi wakati wa msimu wa 2022/23.

Makala haya yanawatazama wachezaji watano ambao walipaswa kujumuishwa kwenye tuzo hizo.

### Bruno Guimaraes
### Klabu: Newcastle United

Msimu wa ajabu wa Newcastle United huenda ambao umewafanya kurejea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kukosekana kwa miaka 20 na sehemu kubwa ya sifa zinahitaji sio tu kufuata njia ya kocha Eddie Howe na wachezaji kama Kieran Trippier na Alexander Isak, lakini kwa kiungo Bruno Guimaraes.

The Magpies hao walijua wamesajili mchezaji maalum katika dirisha la uhamisho la Januari 2022 na msimu huu umeshuhudia Howe akifungua sifa zote kwenye mchezo wa Bruno. Mbrazil huyo amekuwa mchezaji muhimu katikati ya uwanja, akiinua viwango vya uchezaji vya wale wote walio karibu naye huku akitoa sauti kwa kupapasa mpira kwa utulivu.

Uthabiti na uwezo wa Bruno wa kudhibiti michezo umekuwa mkubwa kwa Newcastle na kusema ukweli alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa kikosi hicho. Na katika dunia ya sasa tunayoishi kwa takwimu, ni wazi kwamba, Bruno alistahili kuwepo kwenye tuzo.

### William Saliba
### Klabu: Arsenal

Changamoto ya Arsenal ya ubingwa wa Ligi Kuu ya England inaweza tu kupendeza kwa sababu ya kile kilichotarajiwa kutoka kwao kabla ya msimu mpya kwani malengo yao yalikuwa ni katika nne bora chini ya Kocha Mikel Arteta.

Arsenal sasa wanamaliza ligi wakiwa nafasi ya pili nyuma ya Manchester City, lakini mambo yangekuwa tofauti sana kama William Saliba angeendelea kuwa fiti.

Badala yake, Mfaransa huyo alipata jeraha la mgongo katika mechi ya Arsenal ya Ligi ya Europa dhidi ya Sporting CP, na hajaonekana tangu wakati huo.

Washikabunduki hao wamevuna pointi 15 pekee kati ya 27 zinazowezekana kwa kipindi alichokosekana, wakishinda michezo minne pekee kati ya tisa - licha ya ustadi wa Saka, Odegaard na Gabriel Martinelli, lakini imeonesha jinsi gani Saliba alivyokuwa muhimu. Na zuri zaidi kwao ni kwamba wamefuzu kucheza Ligi ya mabingwa Ulaya msimu judo.

### Mohamed Salah
### Klabu: Liverpool

Mambo yamekuwa magumu. Liverpool imeshindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, kwa sababu ya kiwango duni na matatizo yao mengi yanaweza kusababishwa na majeraha na safu dhaifu ya kiungo.

Salah amekuwa mchezaji pekee ambaye Liverpool wameweza kumtegemea, na mchango wake wa mabao 29 (mabao 19 na pasi za mabao kumi) ni wa pili baada ya Erling Haaland. (Hii ni kabla ya mechi ya mwisho jana Jumapili).

### Declan Rice
### Klabu: West Ham

Mambo si mazuri haswa kwa West Ham kwa mtazamo wa haraka kwenye jedwali la msimamo wa Ligi Kuu, lakini kuna mshangao kwamba Declan Rice hayupo kwenye kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya Mchezaji Bora Chipukizi wa Msimu.

Hapana, si kweli kwamba tuzo zinazotolewa huwa zinalenga timu zinazofanya vizuri tu. (Scott Parker alitwaa tuzo ya Mwanasoka Bora wa Mwaka wa FWA 2011 katika timu iliyoshuka daraja ya West Ham).

Lakini inaweza kuwa rahisi kutoa hoja binafsi kwa Rice kuteuliwa. West Ham wamepoteza mechi 19, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amekuwa bora kabisa msimu mzima - isingewafanya Manchester City, Arsenal, Chelsea, Manchester United na Liverpool zote zinazotaka kumsajili kama angefanya vizuri.

Amepiga pasi nyingi zaidi msimu huu (62), idadi ya tatu kwa juu ya pasi na amekuwa na kiwango bora cha 9/10 katika kila mchezo.

### Rodri
### Klabu: Manchester City

Mbio za Manchester City za kutwaa taji la tatu mfululizo la Ligi Kuu England zilichangizwa na Erling Haaland, Kevin De Bruyne, Ilkay Gundogan na hata John Stones.

Lakini mmoja wa magwiji wa City ambaye hajaimbwa amekaa kwenye safu ya kiungo kwa kipindi bora zaidi cha misimu minne, akiweka sawa mambo huku wachezaji wa klabu hiyo waliochangamka zaidi wakifanya biashara hiyo mbele kidogo.

Hiyo haimaanishi kuwa Rodri hana sifa katika nafasi ya tatu ya mwisho - ameibuka na bao la kipekee la hapa au pale - lakini ustadi wake umesaidia zaidi kuwaweka City katika udhibiti kamili - jambo ambalo Mhispania huyo alilifanya kuwa rahisi.

Lewis Dunk pekee ndiye aliyemaliza pasi nyingi za Ligi Kuu kuliko Rodri katika msimu wa 2022/23, na hakuna aliyepiga pasi zinazoendelea zaidi hadi tatu ya mwisho kama yeye.

## Nukuu

"Ni wakati wa kushangaza na kutia wazimu, niliwaza ingeweza kutokea lakini sikufikiria ingetokea, watu wanapenda mpira na wanaweza wakawa na hisia kuwa hatukustahili kwa sababu mzunguko wa pili wa ligi haukuwa mzuri kwetu, hata hivyo tumefanikiwa kutwaa ubingwa," **Mshambuliaji na Nahodha wa Bayern Munich, Thomas Muller akizungumzia namna timu yake ilivyotwaa ubingwa mbele ya Borrusia Dortmund.**



"Mashabiki wa Tottenham naamini hawatachukulia vibaya, lakini ukweli katika klabu zote nilizowahi kufundisha Spurs ndio klabu ambayo sikuwa na uhusiano nao mzuri nikiwa pale, labda kwa sababu ya mlipuko wa Covid 19 uliofanya uwanja kuwa mtupu wakati wa mechi, lakini sikuwa na uhusiano mzuri," **Kocha Jose Mourinho akiizungumzia timu yake ya zamani aliyofundisha kwa miezi 17 pekee kwenye Ligi Kuu England.**



"Nafahamu Marcus Rashford mkataba wake unamalizika msimu ujao wa 2023/2024, lakini naamini na natarajia kumuona akiongeza mkataba mwingine wa kuendelea kumbakisha hapa Old Trafford, ni mchezaji mzuri na mwenye uwezo mkubwa". **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag akizungumzia mustakabali wa mshambuliaji wa timu hiyo, Marucus Rashford.**





MAYELE

# REKODI, TAKWIMU ZA LIGI KUU KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

ZIMEBAKI raundi mbili tu Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23 umalizike huku Yanga ikiwa imeshatangaza ubingwa.

Hii ni mara ya pili mfululizo kutwaa ubingwa huo, huku ikipata tena nafasi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Wakati zimebaki raundi hizo, timu zitakazoiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao zimeshapatikana, timu hizo ni Simba itakayoungana na Yanga kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, Azam na Singida Big Stars zitaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kuingia fainali ya Kombe la FA, kati ya Yanga na Azam kumechangia timu itakayoshika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu kushiriki michuano hiyo.

Tayari timu moja imeshateremka daraja kati ya timu tatu zinazotakiwa kushuka, nayo ni Ruvu Shooting, huku nyingine ikitarajiwa kushuka moja kwa moja, na zitakazoshika nafasi ya 13 na 14 zitacheza mechi za mchujo, kutafuta timu moja itakayokwenda kucheza mchezo wa mchujo na timu kutoka ligi daraja la kwanza 'Championship'.

Mpaka hapa ligi ilipofikia klabu mbalimbali zimeweka rekodi na takwimu mbalimbali nzuri na mbaya, huku wachezaji pia wakitengeneza rekodi zao.

Mwandishi wa makala haya amekusanya rekodi na takwimu ambazo zimewekwa kwa mtindo wa namba.

**74 -** Ni pointi za mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga walizonazo ikiwa tayari wameshatawazwa kabla ligi haijamalizika.

**67-** Hizi ni pointi za mshindi wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara Simba ambazo hazitafikiwa na timu yoyote, zikimpa tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

**66-** Hii ni idadi ya mabao ambayo Simba imefunga kwenye ligi mpaka sasa, ikiwa ni timu inayoongoza kwa kufunga mabao mengi zaidi mpaka sasa kabla ya mechi mbili za kumaliza msimu.

**56 -** Namba hii inasimama kama ni mabao ya kufunga ya Yanga ambayo tayari imetwaa ubingwa na inashika nafasi ya pili kwa kufunga mabao mengi kwenye ligi mpaka sasa.

**53** - Azam FC ina idadi ya pointi hizi ikishika nafasi ya tatu mpaka sasa kwenye ligi, ikiwa imejihakikisha kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao hata kama ikimaliza kwenye nafasi ya nne.

**51-** Pointi hizi ni za Singida Big Stars iliyopo kwenye nafasi ya nne, nayo ikiwa imeshajihakikishia kucheza Kombe la Shirikisho msimu ujao.

**45 -** Ni idadi ya mabao ya kufunga ya Azam FC, timu inayoshika nafasi ya tatu kwa kufunga mabao mengi mpaka sasa kwenye ligi.

**44-** Mtibwa Sugar ndiyo timu iliyoruhusu mabao mengi zaidi kuliko yoyote ile kwenye Ligi Kuu na hii ni idadi ya mabao hayo.

**40 -** Ni idadi ya mabao ya kufungwa ya timu mbili za Mbeya City na Polisi Tanzania zinazoshika nafasi ya pili kwa kuruhusu wavu wao kuguswa mara nyingi mpaka sasa.

**39 -** Timu ya Namungo inayoshika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ina idadi hii ya pointi kabla ya kumalizia mechi zake mbili zilizobaki.

**37-** Ni mabao ya kufungwa ya Dodoma Jiji ambayo inashika nafasi ya 11 kwenye msimamo ya ligi ikiwa na pointi 31.

**36 -** Prisons iliyo kwenye nafasi ya nane ya msimamo imefungwa idadi hii ya mabao mpaka sasa kwenye ligi ikiwa na pointi 34.

**35 -** Ni pointi za Kagera Sugar ambayo ipo kwenye nafasi ya saba ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**33 -** Timu ya Geita Gold imefunga idadi hii ya mabao na ipo kwenye nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi mpaka sasa.

**30 -** Ni idadi ya mabao ya kufungwa ya timu mbili, Coastal Union inayoshika nafasi ya 10 na KMC ambayo ipo nafasi ya 13.

**29 -** Ni pointi za KMC iliyo nafasi ya 13 na Mtibwa Sugar ambayo ipo kwenye nafasi ya 14 ya msimamo wa Ligi Kuu.

**28 -** Timu zote 16 za Ligi Kuu tayari zimecheza idadi hii ya mechi mpaka sasa.

**22-** Ni idadi ya mabao ambayo Saido Ntibazonkiza ameyachangia kwa kufunga na kutoa pasi za mwisho akiwa na klabu mbili tofauti msimu huu, Geita Gold na Simba.

**16 -** Straika wa Yanga, Fiston Mayele ana idadi hii ya mabao mpaka sasa akiwa ndiye kinara wa upachikaji mabao kwenye Ligi Kuu zikiwa zimebaki mechi mbili msimu kumalizika.

**14-** Clatous Chama wa Simba, anaongoza kuwa na pasi nyingi za mwisho 'asisst' kuliko mchezaji yoyote kwenye ligi, akifuatiwa na Saido ambaye ana 'asisst' 12 mpaka sasa.

**13-** Ni idadi ya mechi ambazo Yanga imeshinda ikicheza uwanja wake wa nyumbani kwa mechi 15 ambazo imecheza, ikiwa inaongoza kwa kushinda mechi nyingi nyumbani kuliko timu yoyote.

**12-** Ni mabao aliyofunga straika wa Yanga, Fiston Mayele akiongoza kwa wachezaji waliofunga mabao mengi kwa mguu huo, akifuatiwa na Jeremiah Juma na Prisons alipachika mabao tisa kwa mguu huo.

11- Simba na Azam kila moja imeshinda kwa idadi hii zikicheza nyumbani. Wakati Simba ikicheza mara 13 nyumbani na Azam imecheza mechi nyumbani mara 14.

**9-** Ni idadi ya mabao aliyofunga kiungo mshambuliaji wa Yanga Stephane Aziz Ki kwa mguu wa kushoto, akiwa ndiye kinara kupachika mabao mengi kwenye ligi kwa mguu huo wa 'dhahabu', akifuatiwa na straika wa Simba, Moses Phiri aliyefunga mabao matano kwa mguu huo katika magoli yake 10 aliyofunga mpaka sasa kwenye Ligi Kuu.

**5-** Mabao ya vichwa aliyofunga straika wa Polisi Tanzania, Kelvina Sabato ambaye ndiye kinara wa kufunga mabao kwa staili hiyo kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**4-** Idadi ya mechi ilizoshinda Dodoma Jiji mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**3-** Ihefu ndiyo timu inayoshika nafasi ya pili kwa kutoa sare chache zaidi mpaka sasa, ikiwa imefanya hivyo kwa idadi hiyo.

**2-** Yanga imetoa sare kwa idadi hii, ikiwa ni timu inayoongoza kwa kutoa sare chache zaidi, lakini pia namba hiyo inasimama kama idadi ya mechi ilizopoteza mpaka sasa.

**1-** Simba inaongoza kwa kupoteza mechi chache zaidi msimu huu kwenye Ligi Kuu, ikipoteza mara moja tu dhidi ya Azam FC kwa kufungwa bao 1-0, Oktoba 27 mwaka jana.

Straika wa Yanga, Fiston Mayele anaongoza mpaka sasa kwa kufunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa na mabao 16, lakini akiongoza kwa kufunga mabao mengi kwa mguu wa kulia, akifanya hivyo mara 12.

**JE, WAJUA?**

WAKATI Simba ikiwa inaongoza kwa kuwa timu iliyofungwa michezo michache kwenye ligi msimu huu, ikifungwa mechi moja pekee na Azam FC Oktoba 27, mwaka jana, kiungo wake Clatous Chama ndiye anayeongoza kwa kuwa na pasi nyingi za mwisho 'asisst' kuliko mchezaji yeyote kwenye ligi, ametoa jumla ya pasi 14 mpaka sasa akifuatiwa na Saido Ntibazonkiza mwenye 'asisst' 12.



# Vyuo vikuu vyatakiwa kuzalisha wataalamu wenye weledi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amevitaka vyuo vikuu vyote nchini kusimamia ubora wa elimu ili kuzalisha wataalamu wenye weledi huku akiwahimiza wahadhiri kujikita kufanya utafiti.

Prof. Mkenda alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapo kwenye uzinduzi wa jengo la utawala la Chuo Kikuu cha Mtakatifu John kwa niaba ya Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango.

Alisema wahadhiri pamoja na kufundisha wafanye utafiti unaotatua kero za wananchi na kuonyesha mchango wao katika sekta ya elimu na serikali imeanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kutoa motisha kwa wahadhiri ambao watafanya vizuri katika utafiti. "Sifa moja ya mhadhiri ni lazima ufanye utafiti ambao utaleta matokeo chanya na sio kukaa kama mwalimu wa kawaida, ilhali unapaswa uibue changamoto na kuzitolea majibu sahihi, mhadhiri asiyefanya utafiti hawezi kuwa mhadhiri na badala yake anakuwa sawa na mwalimu wa kidato cha sita na chuo kikuu kisichofanya utafiti ni sawa na shule ya sekondari," alisema Prof. Mkenda.

Aidha, alisema kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), serikali imekuwa ikitoa ufadhili wa masomo kwa wahadhiri walioajiriwa kwenye vyuo vikuu binafsi ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu vinavyomilikiwa na taasisi za dini.

Alisema hadi sasa wahadhiri 27 wa vyuo vikuu binafsi wamenufaika na ufadhili huo na katika chuo hicho wahadhiri wake watatu wanasomeshwa katika ngazi ya Shahada za Uzamivu nje ya nchi.

Kadhalika, Waziri Mkenda alikitaka chuo hicho kuendelea kupanua zaidi uwezo wa kudahili kwa kuimarisha ubora wa mafunzo na kuongeza miundombinu ya chuo.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Yohana Msanjila, alisema chuo kilikuwa na tatizo la ofisi kwa watumishi na kusababisha wakuu wa idara kuchangia ofisi kinyume na taratibu za usimamizi wa vyuo vikuu.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Prof. Penina Mlama, alisema chuo hicho kimekuwa na mchango mkubwa katika kutoa elimu na hadi sasa kimeshatoa wahitimu 10,002.

Prof. Mlama alimhakikisha Waziri Mkenda kuwa chuo hicho kitaendelea kutoa mchango kwa taifa kwa kuandaa wataalamu katika fani mbalimbali.



Wakazi wa Mtaa wa Mwaja, Kata ya Chamwino jijini Dodoma wakifanya usafi wa mazingira kwenye maeneo ya makaburi yaliyopo Hijra jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC ataka miradi Mkalama kukamilika kabla Juni 30

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewaagiza watendaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, wanaosimamia miradi inayotekelezwa wilayani humo kukamilika yote kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Aidha, ameagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupeleka huduma ya umeme maeneo ya miradi ya ujenzi wa shule mpya za msingi kupitia fedha za BOOST ili kazi ya ujenzi ifanyike usiku na mchana.

Serukamba alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara ya siku mbili kukagua miradi ya ujenzi wa shule mpya za msingi, zahanati, vituo vya afya, mabweni, madarasa na vyoo ambayo serikali imetoa mamilioni ya fedha kwa ajili ya kuitekeleza.

"Tunaipongeza sana serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeleta fedha nyingi sana kwenye halmashauri, hivyo ambao tumepewa nafasi ya kuwa viongozi kazi yetu ni kuhakikisha fedha hizo zinafanya kazi iliyokusudiwa miradi ikamilike kwa wakati na izingatie 'value for money' (thamani ya fedha)," alisema.

Mkuu wa mkoa alisema moja ya maelekezo mahsusi yaliyotolewa na Waziri Ofisi ya Rais, Tawala Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, ni kuhakikisha kusiwe na bakaa, yaani fedha zinarudi baada ya mwaka mpya wa fedha kwisha badala yake miradi yote inakwisha.

"Mkalama kwenye shule zinazojengwa kwa fedha za BOOST kasi sio nzuri sana ndiyo maana nimempa maelekezo Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ahakikishe kila siku anatembelea miradi na kutoa maelekezo kwa mafundi ili miradi ikamilike Juni 20, mwaka huu," alisema.

Serukamba alisema kuanzia sasa kazi ya ujenzi wa miradi hiyo iwe inafanyika hata siku za Jumamosi ili kukimbizana na muda kwa kuwa hatapenda kuona baada ya Juni 30 fedha zinarudishwa serikalini kwasababu miradi haijakamilika.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mkalama, James Mkwega, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kwamba miradi yote katika wilaya hiyo itamalizika kwa muda uliopangwa.

## Mradi wa kidijitali kuimarisha utoaji huduma

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Benedict Ndomba, amesema mradi wa kidijitali (Digital Tanzania), unatarajiwa kuimarisha utoaji wa huduma kwa njia ya kidijitali na kuchochea uwekezaji nchini.

Ndomba aliyasema hayo juzi jijini hapa baada ya kufanyika kikao cha majadiliano ya mradi huo ambao utekelezaji wake unaendelea.

Mkurugenzi huyo alisema mradi huo una malengo makuu mawili ambayo ni kuongeza upatikanaji wa huduma za mtandao wa intaneti zenye gharama nafuu na ubora wa juu kwa serikali, wafanyabiashara na wananchi sambamba na kuboresha uwezo wa serikali wa kutoa huduma za umma kidijitali.

"Lengo la pili la mradi huo ni kuchangia upatikanaji wa intaneti na huduma za umma kidijitali ili kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika miradi ya kidijitali na kuongeza ajira," alisema Ndomba.

Alifafanua kuwa kupitia mradi huo e-GA inayo majukumu matatu ambayo ni upanuzi wa mtandao wa serikali, uboreshaji wa vituo vya kuhifadhia data pamoja na masafa ya intaneti (bandwith) na vituo 660 vinatarajia kunufaika.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, unatekelezwa kwa usimamizi wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zinazohusika na TEHAMA ikiwamo e-GA.



# Mitambo 60 ya kuchakata kahawa yakarabatiwa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SHIRIKA la Café Africa Tanzania, limekarabati mitambo 60 ya kuchakata kahawa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2023 kupitia mradi wa kuendeleza zao hilo (Coffee development project (CO-DEP).

Mradi huo ambao uko chini ya programu ya AGRI-CONNECT, unatekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Songwe na Ruvuma, imekuwa msaada mkubwa katika kuwawezesha wakulima wa zao la kahawa kunufaika na kilimo chao kwa kujengewa uwezo na namna ya kuzalishaji iliyo bora na kuongeza thamani.

Meneja mradi wa kuendeleza zao hilo mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya, Ruvuma na Songwe CO-DEP, Emmanuel Mahululu, alisema msimu wa kilimo mitambo 40 katika msimu wa kilimo 2020/2021 na 2021/2022 na msimu wa 2022/2023 mitambo 20 itakarabatiwa.

"Lengo la mradi huu ni kuchangia maendeleo endelevu ya zao la kahawa katika mnyororo mzima wa thamani kwa kuongeza kipato na kuboresha lishe miongoni mwa wakulima wadogo wa zao la kahawa na unatekelezwa na mashirika ya VI-Agro forestry kama shirika kiongozi, TaCRI, Café Africa Tanzania, Brac Maendeleo na ANSAF," alisema Mahululu na kuongeza,

"Café Africa Tanzania kupitia mradi wa CO-DEP hadi Aprili 2023, watumewafikia wakulima 20,508 wa mikoa mitatu tunayofanya nayo kazi ambao kati yao 6,519 ni wanawake na 3,989 ni wanaume miaka mitatu ya mradi wetu," alisema Mahululu. Alisema kuwa lengo la mradi huo ni kuwafikia wakulima 24,000 kabla ya mradi kumalizika na wataendelea kupatiwa mafunzo ya kilimo bora cha kahawa kwa wakulima wa wilaya za Mbozi, Ileje, Rungwe, Mbeya, Mbinga na Nyasa.

Katibu Tawala Uchumi na Mipango wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alipongeza jitihada zinazofanywa na shirika la Café Africa ambao wamewasaidia wakulima kuwapatia elimu ya usimamizi wa kahawa baada ya kuvuna hasa mbinu za kuzingatia baada ya kuchuma kahawa shambani.

Uchakataji wa kahawa mbivu kwa ujumla, mafunzo ya jinsia kwa kushirikisha wanawake na vijana kwenye mnyororo wa thamani wa zao la kahawa ikiwa ni pamoja na uundaji wa vikundi vya vijana, kuhamasisha suala la uthibitishwaji kwa zao la kahawa, mafunzo ya masoko maalum. Elimu nyingine ni uongezaji thamani wa zao la kahawa, mafunzo ya uongozi na utawala bora katika vyama vya ushirika na ukarabati wa miundombinu ya mitambo ya kuchakata kahawa.

"Mradi huu Cafe Africa Tanzania imewaleta wadau wa jukwaa la kahawa katika masoko na uongezaji wa thamani wa zao hilo ambapo iliwakutanisha wakulima wadogo wa kahawa, Serikali, Bodi ya Kahawa Tanzania, kampuni, mashirika na sekta binafsi kwa pamoja ili kujadili fursa za masoko, uongezaji thamani wa zao hilo na masoko, kubadilisha na uzoefu ili kuongeza ushirikiano miongoni mwa wadau wote walioko kwenye mnyororo wa thamani," alisema Madito.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Mapendo kilichopo wilayani Mbinga Mkoa wa Ruvuma, Yasint Wello, alisema kuwa Café Africa imempatia kila mkulima miche 500 ya kahawa ili kupanda shambani kwake.



Waziri wa Afya na Mbunge wa Tanga, Ummy Mwalimu, akimfariji mgonjwa aliyelazwa katika Kituo cha Afya Makorora jijini Tanga juzi, ikiwa ni ziara aliyoifanya na viongozi wa CCM, walishiriki kufanya usafi katika kituo hicho ili kuweka mazingira salama kwa kujiepusha na magonjwa yanayoambukiza. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wateja watakiwa kulipa bili za maji kwa wakati

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Jiji la Mbeya, (MBEYA UWSA), imewataka wateja wake kulipa ankara ya maji kwa wakati ili kuiwezesha mamlaka hiyo kutoa huduma bora na kwa wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, CPA Gilbert Kayange, alisema, ulipaji wa Ankara za maji kwa wakati utasaidia kuboresha huduma ikiwamo upatikanaji wa maji muda wote.

Alisema hamasa hiyo ni sehemu ya mpango biashara ya UWSA, wamedhamiria kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira ikiwamo utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji ambayo inatokana na fedha za ndani na serikali kuu.

"Ili mamlaka iendelee kutoa huduma ni lazima wateja, zikiwamo taasisi za umma kulipia ankara ya maji kwa wakati kwa kuwa shughuli zake ikiwamo mpango biashara unategemea fedha," alisema CPA Kayange.

Hivi karibuni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Edina Mwaigomole, alisema wanaendelea kuwakumbusha wadaiwa wote sugu wenye malimbikizo ya madeni.

Alisema taasisi za umma ni miongoni mwa wadaiwa na kwamba tayari baadhi zimeanza kulipa madeni, aliwakumbusha wadeni wote kulipa ankara za maji ili kusaidia utoaji mzuri wa huduma za maji.

Miongoni mwa wananchi walilalamikia baadhi ya watumishi wa idara hiyo kubambikizia wateja bili za maji ikilinganishwa na hali halisi ya utumiaji wa maji kwa mwezi.

Alisema mamlaka hiyo inajipambanua kufanya kazi vizuri, lakini baadhi ya watendaji sio waaminifu wakitaka kiasi kikubwa cha fedha ili waziweke mfukoni.

# RC ahamasisha h'shauri uchangiaji ujenzi mabweni

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameziagiza halmashauri za mkoa huo, kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndaki ya Mzumbe.

Homera alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipoongoza harambee ya kuchangia ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike wa chuo hicho na kwamba Sh. bilioni 4.5 zinahitajika ili kukamilisha ujenzi huo ambao utawasaidia wanafunzi hao kusoma kwenye mazingira ya usalama.

Alisema uwapo wa Chuo cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya ni fursa ya kiuchumi kwa sababu wafanyabiashara wanajiingizia kipato kutokana na uuzaji wa vyakula, nguo na mahitaji mengine muhimu ya kibinadamu.

Kutokana na hali hiyo alisema ni vyema halmashauri zote za wilaya ambazo zinanufaika moja kwa moja na chuo hicho ambacho kinapokea wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali nchini.

"Nafurahi Naibu Meya upo hapa sasa natumia fursa hii kuziagiza halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya, kuchangia ujenzi wa mabweni ya chuo chetu, mtaangalia mnafanyaje, lakini 'focus' yetu ni kuhakikisha jengo hilo linakamilika kwa wakati ili wanafunzi wetu hasa wasichana wasikumbane na vikwazo," alisema Homera.

Homera aliahidi kuchangia Shilingi milioni sita ili kusaidia ujenzi huo huku akiwahamasisha viongozi wengine kusaidia.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa William Mwegoha, alisema kwa sasa chuo hicho kina hosteli ya kubeba wanafunzi 410 kati yao wanawake ni 260 idadi ambayo ni ndogo ukilinganisha na wanafunzi waliopo ambao ni 34,011.

Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Henry Molel, alisema kukamilika kwa hosteli hizo kutasaidia kubeba wanafunzi wa kike 800 ambao wataishi mazingira ya shule.

Agripin Boniface, mwanafunzi wa Chuo hicho alisema wanapitia vikwazo mbalimbali wanapoishi nje ya shule ikiwamo kuibiwa, kushawishika kuingia kwenye vitendo vinavyoharibu ndoto zao kama vile ulevi na umalaya.

Alisema kukamilika kwa hosteli hiyo kitasaidia kuwa karibu na shule na muda mwingi watautumia kusoma ili kufikia ndoto zao.



## Mawaziri wa Fedha Bara, Visiwani wakutana kujadili kodi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Fedha na Mipango Zanzibar na Wizara ya Fedha na Mipango Tanzania Bara, chini ya mawaziri wake Dk. Saada Salum Mkuya na Dk. Mwigulu Nchemba, zimekutana visiwani Zanzibar kujadili masuala ya kikodi ambayo yanatekelezwa katika pande mbili za Muungano wa Tanzania.

Kikao hicho cha majadiliano kimefanyika mwishoni mwa wiki katika Ofisi za Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na kuwashirikisha wataalamu wa taasisi za kikodi ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na wizara mbili za fedha Zanzibar na Tanzania bara.

Akizungumza katika kikao hicho, Waziri Saada alisema, uchumi na fedha katika pande za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaingiliana kupitia taasisi za kikodi, kisera na uchumi wa jumla na kwa pamoja zinaendeshwa na taasisi za Muungano ikiwamo Benki Kuu ya Tanzania.

Alisema lengo la kikao hicho ni kuangalia maeneo yatakayorahisisha kufanyika kwa biashara katika pande mbili za Muungano hasa ikizingatiwa kuwa kuna wafanyabiashara wanaotoka Zanzibar kwenda Bara kufanya biashara na wa Bara kufika Zanzibar kufanyabiashara. Alisema katika ufanyaji wao wa biashara kuna mambo yanayowakwaza ikiwamo masuala ya marejesho ya ongezeko la thamani (VIT) na ulipaji wa kodi na baadhi ya wafanyabiashara wanalalamika kulipa kodi mara mbili hivyo ni vyema kuweka mifumo mizuri ili kuondoa changamoto hiyo na kurahisisha ufanyaji wa biashara.

"Sasa hivi Bunge linajadili bajeti ya serikali, lakini vile vile, Baraza la Wawakilishi linajadili bajeti ya serikali, tunakwenda kusoma bajeti kuu za serikali Juni 15, mwaka huu na hamu kubwa ya Watanzania wanayopenda kusikia ni maeneo ya kikodi, vipi serikali zinaweza kuweka mazingira mazuri ya kikodi," alisema Dk. Mkuya.

Waziri Dk. Nchemba, alisema viongozi wakuu wa nchi, Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Hussein Ali Mwinyi wanaelekeza kutengeneza mazingira mazuri ya biashara ili kuwavutia wawekezaji na kikao hicho cha majadiliano ni muhimu.

Aidha, alisema kikao hicho kitajadili masuala ya kiutawala katika usimamizi wa sera za kikodi na kuwahakikishia wananchi kuwa serikali ipo makini inatengeneza mazingira bora na wananchi kufanya biashara, kuvutia uwekezaji na wananchi kujiajiri na kuweka maisha mazuri kwa kila Mtanzania.

# Polisi kuchunguza mauaji ya wasichana 2 Mjini Magharibi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar, limesema linaendelea kufanya uchunguzi wa matukio mawili ya mauaji ya wasichana yaliotokea Mei 20, mwaka huu katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Richard Mchomvu, alisema tukio la kwanza lililotokea huko Kijichi katika nyumba yenye usajili H/K208, msichana Laura Bitrim Msemwa (23) alikutwa amefariki ndani ya chumba chake katika nyumba hiyo aliyopanga.

Alisema tukio hilo limegundulikana baada ya wapangaji wezange kusikia harufu kali kutoka ndani ya chumba cha msichana huyo. Kamanda alisema kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa majirani zake, siku mbili kabla ya tukio hilo msichana huyo aliwataarifu wenzake kuwa atakua na mgeni wake ambaye atafika hapo.

"Ni kweli huyo mgeni wake alifika ambaye ni kijana wa kiume akiwa amevaa kanzu na barakashia na walikaa ndani kwa muda ambapo majira ya saa 10 jioni kijana huyo alitoka na kufunga mlango kwa nje na siku ya pili kijana huyo alirejea tena bila ya msichana kumuona kwa siku mbili," alisema.

Alisema majirani hao waliingiwa na hofu baada ya siku ya tatu kusikia harufu kali ikitoka ndani ya chumba na kulijulisha Jeshi la Polisi ambalo lililazimika kuvunja mlango na kumkuta msichana huyo akiwa ameshafariki bila ya kuwa na majeraha. "Tulikuta mwili wa marehemu umeshaharibika usoni akiwa yupo kitandani bila ya kuwa na majeraha, lakini tulikuta vinywaji mezani katika chumba hicho na inaoneka kama walikuwa wakinywa na huyo aliyekuwa naye," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ili kujua kifo cha msichana huyo na aliyefanya uhalifu huo ili sheria ichukue mkondo wake.

"Tupo vizuri na tunafuatilia kwa ukaribu tukio hili na tutajua tukio hili limetokana na nini na sheria kuchukua mkondo wake, imani yetu kuwa kifo chake kimetokana na mazingira ya unywaji na tunaamini huyo kijana aliyekuwa naye ni mtu wanayefahamiana," alisema. Aidha, alisema tukio lingine lililotokea siku hiyo hiyo ya Mei 20 majira ya saa nne asubuhi, Jeshi la Polisi lilipata taarifa ya kukutwa kwa mwili wa msichana Khairat Juma Bakari (28), mkaazi wa Donge, katika boma la nyumba huko Mbuzini Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, mwili wake ukiwa umeharibika kwa kuchomwa na vitu vyenye ncha kali.

Alisema uchunguzi wa awali umetambua nyumbani kwao alipokuwa akiishi na kabla ya tukio hilo alikwenda benki kutoa fedha kiwango kikubwa, lakini nyumbani kwao hakufika na kukutwa katika eneo hilo akiwa ameshafariki.

"Uchunguzi unaendelea, lakini ninachowaambia wananchi matukio haya yamebainika siku moja lakini hayajatokea siku moja na mazingira yake ni tofauti tunavyoona hili tukio moja yawezekana ikawa ni wivu wa kimapenzi na hili tukio la pili ni ukatili ambao umetokana kwa wahalifu kutaka kujipatia kipato," alisema Kamanda Mchomvu.

Kutokana na matukio hayo asasi za kiraia zinazotetea haki za wanawake na watoto zimelaani vitendo hivyo na kulitaka Jeshi la Polisi kutumia rasilimali zake zote kuwatafuta wahalifu na kuharakisha upelelezi ili kuwafikisha katika vyombo vya sheria mapema iwezekanavyo na hivyo kulipia makosa yao hayo. Jamila Mahmoud, Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA, Zanzibar), Dk. Mzuri Issa, walisema kupatikana kwa haki kutawatisha wahalifu wengine ambao wana nia ya kufanya vitendo hivyo vya kikatili na kuhakikisha kwamba matukio kama hayo hayaendelei kutokea Zanzibar.

"Pia TAMWA na ZAFELA zinaiasa jamii kuacha kutenda vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto ambavyo vinakiuka haki za kibinadamu na kuteteresha ustawi kwa makundi ya wanawake na wasichana," alisema Mzuri.

Wanaharakari hao, walisema nchi ndogo kama Zanzibar kukiwapo na upelelezi na ushirikiano mzuri wa jamii, wahalifu wanaweza kupatikana kwa muda muafaka.

Kwa mujibu rekodi za taasisi hizo tangu mwaka 2016, matukio 23 ya mauaji ya wanawake na watoto yameripotiwa na upatikanaji wa haki umekuwa ni mgumu kufikiwa.



Mbunge wa CCM Jimbo la Malindi, Mohamed Suleiman Omar (wa pili kulia), amekabidhi bodaboda mbili na mashine maalumu ya kusagia vyakula vikavu (viungo) kwa vikundi vya matawi ya CCM, Gulioni na Miti Ulaya vyenye thamani ya Sh. milioni 7,200,000. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# 'Wenye ulemavu wanaendelea kutengwa, kubaguliwa'

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya jitihada za serikali kwa kushirikiana na jumuiya mbalimbali zinazoshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu kukemea vitendo vya udhalilishaji kwa watu hao, lakini bado hutengwa, hubaguliwa na kutendewa ukatili.

Hayo yalisemwa visiwani hapa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, wakati akifungua mafunzo kwa viongozi wa Serikali za Mitaa, wakiwamo wakuu wa wilaya na mikoa, Makamanda wa Polisi wa mikoa na wilaya kuhusu uzingatiaji wa masuala ya watu wenye ulemavu Zanzibar.

Othman alisema hatua hiyo inafuatia masuala ya watu wenye ulemavu kupewa kipaumbele ulimwenguni baada ya kubainika kundi hilo ambalo ni sehemu ya jamii kukosa haki zake za msingi na kusababisha Umoja wa Mataifa kuanzisha mkataba wa watu wenye ulemavu duniani.

Alisema katika kutekeleza mkataba huo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imechukua jitihada za kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki na fusra wanazostahiki ili waendelee kuishi vyema kama wengine.

Alizitaja miongoni mwa jitihada hizo kutungwa sera ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2008 na kutungwa kwa sheria mpya inayosimamia masuala ya watu hao ya mwaka 2022, Zanzibar.

Aidha, aliwataka wakuu wa wilaya kuzingatia kifungu namba nane cha sheria hiyo kwa kuanzisha na kuyasimamia Mabaraza ya watu wenye ulemavu ndani ya wilaya zao ili kufikia malengo ya kuwapa huduma bora watu wa jamii hiyo.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak, alisema kwamba mafunzo hayo ni mwendelezo na jitihada za serikali kupitia ofisi hiyo katika kuifanya jamii na viongozi kuwa na uelewa kuhusu masuala yote ya watu wenye ulemavu.

# Katibu Mkuu Kiongozi ataka ARU iwe kimataifa

**Na Joseph Mwendapole**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Dk. Moses Kusiluka, amesema serikali inatamani kuona Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) kinakuwa sehemu ya jumuiya ya kimataifa kwa kutoa elimu yenye viwango vya kimataifa na kuvutia wanafunzi wengi kutoka nje ya nchi.

Amesema chuo hicho kinapaswa kuendelea kutoa wahitimu bora watakaoshindana katika soko la ajira la ndani na nje ya Tanzania.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa sherehe za uzinduzi wa Kamati ya Ushauri ya Kisekta ya chuo hicho iliyobuniwa chini ya mradi wa HEET.

Alisema ARU inapaswa kuwa kituo cha umahiri katika uvumbuzi na utafiti, methodolojia na teknolojia zitakazowezesha utoaji wa huduma bora kwa jamii, hivyo kuchangia katika utatuzi wa migogoro mingi hususani inayoendana na usimamizi wa sekta ya ardhi.

Dk. Kusiluka alisema chuo hicho pia kinapaswa kuchangia katika kuongeza mapato ya serikali kwa kubuni miradi mbalimbali ya utafiti, ushauri wa kitaalamu na taaluma na hivyo kupunguza mzigo wa uendeshaji wa taasisi za elimu ya juu.

Kwa mujibu wa Dk. Kusiluka, ARU inapaswa kutoa mchango stahiki kwa serikali na taifa hususani katika masuala ya utayari wa majanga, suluhisho baada ya majanga kutokea na kujenga uwezo himilivu kwa jamii ya Watanzania katika kukabiliana na majanga hayo.

Naibu Makamu Mkuu wa chuo hicho anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri, Prof. John Lupala, alisema mradi huo unatekelezwa kwa kushirikisha vyuo 14 vya umma, taasisi tatu za elimu ya juu na vyuo vitano ambavyo viko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Alisema kamati itakuwa na kazi ya kutoa mapendekezo yatakayosaidia chuo kutatua changamoto za ajira, kuchambua na kushauri kuhusu mahitaji ya soko la ajira, kufafanua na kutangaza huduma nyingine ambazo chuo kinatoa.

Alisema kamati itakuwa kiunganishi kati ya chuo na jamii na kutoa mapendekezo kwa chuo kuhusu fursa za ushirikiano na vyuo vingine.

Alisema HEET ni mradi wa miaka mitano unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na kuratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Prof. Lupala alisema ARU ni mnufaika wa mradi huo na chuo kimepata dola za Marekani milioni 29 (Sh. bilioni 68.2).

Alisema mradi huo unalenga kukijengea uwezo chuo katika mambo mbalimbali, ikiwamo kuongeza kiwango cha udahili wa wanafunzi na kuboresha mitaala ya kufundishia ili kuendana na mahitaji ya soko katika programu za kipaumbele za mradi.

Alitaja eneo la kwanza kuwa ni ujenzi na uboreshaji wa miuondombinu ambapo majengo manne ya madarasa, maabara, studio na karakana za ufundi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,712 na wakufunzi na wafanyakazi 143 yatajengwa katika Kampasi ya Dar es Salaam.

Alisema baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Kampasi ya Dar es Salaam, chuo kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 11,323 ambalo ndilo lengo la chuo katika kipindi cha miaka saba ijayo.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Balozi Salome Sijaona, aliwashukuru wajumbe wa kamati kwa kukubali uteuzi wa kuchukua jukumu la kuwa washauri wa chuo hicho kwa huduma ambazo chuo kinazitoa kwa jamii.

Alisema huduma hizo zinajumuisha kutoa elimu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa jamii na kupitia ushauri wao anaamini chuo kitapiga hatua kubwa katika kuchangia maendeleo ya nchi.




Baadhi ya wateja wakipatiwa huduma na wafanyakazi wa Vodacom Tanzania katika duka jipya baada ya kuzinduliwa na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa (hayupo pichani), linalopatikana Aim Mall jijini humo. Mkuu huyo wa Wilaya alisisitiza umuhimu wa ufanisi na ubora hasa katika kuchochea huduma za mawasiliano vijijini pamoja na kuchochea shughuli za utalii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TIB yatoa mkopo uzalishaji nishati

**Na Seleman Mpochi**

BENKI ya Maendeleo ya TIB imeunga mkono juhudi za uzalishaji wa nishati nchini kwa kutoa mkopo wa zaidi ya dola za Marekani 400,000 kwa Kampuni ya Nishati Lutheran (DKK) Investment Ltd inayotekeleza Mradi wa Umeme wa Ijalanga 'Small Hydro Eclectic Power Project (ISHEP)' pembezoni mwa Mto Ijawala mkoani Njombe.

Mwishoni mwa wiki, Mwakilishi wa TIB, Mkurugenzi Mtendaji, Joseph Chilambo, alibainisha hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa mradi huo katika makao makuu ya Kampuni ya DKK Investment Ltd, Kata ya Tandala, Kijiji cha Msisiwe Makete wilayani Njombe.

Chilambo alisema benki imetoa mkopo kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa mradi huo ambao utakuwa na uwezo wa kuzalisha kilowati 360.

Alisema benki imechagua kufadhili mradi huo kwa kuwa unatarajiwa kuwa na matokeo chanya ya kiuchumi na kijamii, ambazo zitachangia mpango wa nchi wa kusambaza umeme vijijini na kupunguza umaskini vijijini kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya uzalishaji umeme, ili kuongeza tija katika shughuli za maendeleo nchini.

Alisema mradi huo utaboresha hali ya maisha kwa kuboresha upatikanaji wa umeme kwa maendeleo ya biashara ndogo na matumizi ya nyumbani.

Mradi wa Umeme wa Ijalala Small Hydro Eclectic Power sasa uko chini ya utaratibu wa Mpango wa Upanuzi wa Nishati Jadidifu Tanzania (TREEP) chini ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA). REA kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB) imeanzisha programu ya kusaidia maendeleo ya miradi ya nishati jadidifu nchini.

TREEP imeundwa kama Programu ya Matokeo (PforR), inayounga mkono Mpango wa Kitaifa wa Umeme Vijijini wa Serikali (NREP) kwa kuunganisha kwa ubunifu utoaji wa fedha moja kwa moja na utoaji wa matokeo yaliyoainishwa na kufikia malengo yake, ambayo ni pamoja na kupanua upatikanaji wa umeme vijijini.

# BoA kuwezesha makandarasi katika utekelezaji wa miradi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Afrika (BoA) Tanzania imewahakikishia makandarasi nchini upatikanaji wa mikopo na dhamana za benki ambazo zitawarahisishia vigezo vya kupata mikataba na kufanikisha miradi yao.

Meneja wa Kitengo cha Utoaji Fedha za Biashara wa benki hiyo, Jessica Mizambwa, alibainisha hayo wakati benki hiyo iliposhiriki Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Bodi ya Wasajili wa Makandarasi jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

"Benki inatoa huduma maalum ambazo ni suluhisho katika kufadhili miradi mbalimbali ya makandarasi. Huduma hizo zinazotolewa na benki yetu ni pamoja na dhamana ya zabuni inayotoa dhamana ya hadi Sh. bilioni moja ndani ya saa 24.

"Pia tuna dhamana ya malipo ya mapema, dhamana ya utendaji kazi, punguzo la ankara, mikopo na nyinginezo na zinapatikana kwa haraka," alisema Jessica.

Alisema huduma za kifedha kusaidia biashara zinalenga kukuza ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi kwa kuwezesha usafirishaji wa bidhaa kuvuka mipaka na hata ndani.

Hivyo, benki inawezesha wafanyabiashara wa aina mbalimbali wakiwamo makandarasi, waagizaji bidhaa kutoka nje na wauzaji bidhaa nje ili kupunguza uwezekano wa kupata hasara zinazohusiana na kufanya biashara za nje ya nchi.

Jessica aliongeza kuwa kupitia mpango wa benki wa kuwezesha makandarasi, hasa wadogo, wanaweza kupata mashine bora za kufanyia kazi na kufanikisha kutekeleza miradi yao.

"Bank of Africa Tanzani itawawezesha makandarasi kupata mashine na kuondoa tatizo la makandarasi kushindwa kutoa huduma kwa kukosa mashine au fedha," alisisitiza.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, aliwataka makandarasi wazawa nchini kuwa mabalozi wazuri kwa kufanya kazi nzuri kwa kuzingatia viwango na kukamilisha miradi kwa wakati ili serikali ipate thamani ya fedha katika miradi yote.

Kasekenya alisema makandarasi wana mchango mkubwa katika kuinua uchumi wa nchi na inapotokea wanashindwa kutimiza wajibu wao, wanachelewesha wananchi kupata huduma zilizokusudiwa na kuisababishia hasara serikali.

HABARI KIMATAIFA

# Mbaroni kwa wizi wa maiti 31 Marekani

**INDIANA,** Marekani

MKURUGENZI wa mazishi katika jimbo la Indiana nchini Marekani, Randy Lankford, ametiwa hatiani baada ya eneo lake kukutwa na miili iliyoharibika ya watu zaidi ya 31, huku akikiri makosa mengine 40 ya wizi.

Kwa mujibu wa BBC, waendesha mashtaka walimshtaki Randy Lankford, ambaye anamiliki biashara ya mazishi huko Jeffersonville, kwa kushindwa kukamilisha shughuli za mazishi alizolipwa.

**Lankford amewekwa chini ya kizuizi cha nyumbani hadi hukumu yake itakapotolewa.**

Kutokana na maelezo ya jaji anayesimamia kesi hiyo, Lankford anaweza kutumikia miaka 12 na kupewa amri ya lazima ya kufidia familia 53 dola 46,000 alizolipwa kwa ajili ya shughuli ya mazishi.

Ilielezwa kuwa Lankford atahukumiwa Juni mwaka huu, na kwamba Polisi wa Jeffersonville walianza kuchunguza Kituo cha Mazishi cha Lankford na Kituo cha Familia Julai 2022 kutokana na ripoti za kuwepo kwa harufu kali kutoka kwenye jengo lake.

"Miili hiyo ambayo haikuhifadhiwa kwenye jokofu ilipatikana katika hali mbalimbali za kuoza kwani baadhi walikuwa kwenye nyumba ya mazishi kwa miezi kadhaa," ilisema taarifa ya polisi.

"Mabaki ya maiti ya watu 17 pia yalipatikana. Lankford amewekwa chini ya kizuizi cha nyumbani hadi hukumu yake itakapotolewa," ilisema.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa jaji alipendekeza Lankford akae jela miaka minne na miaka minane chini ya kizuizi cha nyumbani. Vile vile, mwendesha Mashtaka wa Kaunti ya Clark Jeremy Mull alisema kuwa kesi dhidi ya mwanaume huyo mwenye miaka 50 ilikuwa ngumu.

Miongoni mwa madai katika hati za mahakama zilizowasilishwa ni kwamba familia kadhaa zilipokea kile walichoamini kuwa ni majivu ya wapendwa wao.

Pia inaelezwa kuwa baada ya miezi kadhaa waliwasiliana na polisi na kuambiwa majivu halisi yaligunduliwa kwenye nyumba ya mazishi ya Lankford, na kwamba mwanafamilia wao hakuwahi kuchomwa moto. **BBC**



Wafuasi wa kundi la waasi wa M23 ambao serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), imewashutumu kwa kuimarisha ngome zake kwa lengo la kuvamia mji mkuu wa Kivu Kaskazini mwa Goma. **PICHA: MTANDAO**

## Kyiv yakumbwa na mashambulizi

**KYIV,** Ukraine

MAOFISA wa Mjini Kyiv, Ukraine wamesema Russia imefanya shambulizi katika eneo hilo usiku wa kuamkia jana na kusababisha kifo na majeruhi mmoja, pamoja na uharibifu wa miundombinu.

Meya wa Kyiv, Vitaliy Klitschko, alisema mtu mmoja alifariki wakati mabaki ya ndege zisizo na rubani zilipoanguka karibu na kituo cha mafuta na mwanamke mmoja pia alijeruhiwa.

Alisema vikosi vya ulinzi wa anga viliangusha zaidi ya ndege 20 zisizo na rubani zilizokuwa zimeelekezwa Kyiv, na kwamba baada ya muda wimbi jipya la ndege zisizo na rubani lilikaribia eneo hilo.

Ilibainishwa kuwa hivi karibuni Russia imeongeza mashambulizi yake dhidi ya Kyiv, ikitaka kuzidisha ulinzi wa mji mkuu huo.

Pia ilielezwa kuwa baada ya shambulio hilo jana tahadhari za uvamizi wa anga zilianzishwa katika mikoa 12 ya Ukraine, kutoka Volyn kaskazini magharibi hadi Dnipropetrovsk kusini mashariki.

Ukraine imekuwa ikipanga kukabiliana na mashambulizi kwa miezi kadhaa, na kwamba imetaka muda mwingi iwezekanavyo kutoa mafunzo kwa wanajeshi na kupokea vifaa vya kijeshi kutoka kwa washirika wa Magharibi.

Katika chapisho kwenye mtandao wa kijamii Klitschko aliwataka wakazi wa Kyiv kukaa katika makazi, akionya kwamba usiku huo utakuwa mgumu.

Alisema majengo mawili ya juu katika wilaya tofauti za mji mkuu yameungua baada ya kugongwa na vipande vya ndege zisizo na rubani zilizoanguka.

Katika mashambulio ya hivi karibuni, Russia ilikuwa ikitumia kinachojulikana kama ndege zisizo na rubani za kamikaze pamoja na safu ya makombora ya cruise na balestiki. **BBC**

## Uchaguzi wa rais wafanyika tena Uturuki

**ANKARA,** Uturuki

WANANCHI Uturuki wamepiga tena kura katika awamu ya pili ya marudio ya kura ya urais ili kuamua kwamba Rais wa nchini humo Recep Erdogan anafaa kubaki madarakani baada ya miaka 20.

Waturuki hao wamepiga kura hiyo kwa awamu ya pili jana baada ya awamu ya kwanza kudaiwa kuwa hakukuwa na usawa.

Mpinzani Kemal Kilicdaroglu, anayeungwa mkono na muungano mpana wa upinzani, aliidhinisha kura hiyo kama kura ya maoni kuhusu mwelekeo wa baadaye wa Uturuki.

Rais ambaye amekuwa akishinda mara kadhaa katika kinyang'anyiro cha urais Uturuki, aliahidi enzi mpya ya kuunganisha nchi huyo karibu na karne ya Kituruki, na kwamba suala kubwa zaidi la kuangaliwa ni mfumuko wa bei uliokithiri na mgogoro wa gharama ya maisha.

Inaelezwa kuwa kura kutoka kwa wageni, iliyofanywa kote ulimwenguni, tayari imekamilika na kwamba waliojitokeza katika awamu ya kwanza walikuwa ni asilimia 88.8 na uongozi wa Erdogan ulipata kura milioni 2.5.

Aidha, ilielezwa kuwa wagombea wote wawili wameelekeza macho yao kwa wananchi milioni nane ambao hawakupiga kura, huku Kilicdaroglu akimshutumu mpinzani wake kwa kuzuia ujumbe wake wa maandishi kwa wapigakura wakati ujumbe wa rais ukipita.

Hata hivyo, inabainishwa kuwa vyama vya upinzani vinatumia jeshi la watu wa kujitolea ili kuhakikisha hakuna wizi wa kura unaofanyika.

Waangalizi wa kimataifa walizungumza kuhusu kutokuwapo usawa baada ya awamu ya kwanza, lakini hakukuwa na pendekezo kwamba makosa yoyote katika upigaji kura yangebadilisha matokeo.

Kilicdaroglu aliahidi mtindo tofauti wa urais katika siku yake ya mwisho ya kampeni, "Sina nia ya kuishi katika majumba, nitaishi kama wewe, kwa kiasi ... na kutatua matatizo yako."

Pia ilidaiwa kuwa baada ya kiongozi huyo kunusurika katika mapinduzi ya mwaka 2016, alichukua mamlaka makubwa na kuweka kizuizini maelfu ya watu na kuchukua udhibiti wa vyombo vya habari.

Inadaiwa kuwa Uturuki ina mgawanyiko wa kisiasa na kwamba rais anaegemea uungwaji mkono wa wafuasi wa kidini na wapenda utaifa, wakati wafuasi wake wa upinzani wengi wao ni wasiopenda dini, licha ya kuwa wengi wao ni wazalendo pia. **BBC**

# ROBERTINHO ATOA NENO KAMATI YA USAJILI SIMBA

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera ameitaka kamati ya usajili ya klabu hiyo kusajili wachezaji wanaolingana kiuwezo ili kupata uwiano sahihi pindi mmoja anapokosekana.

Kamati ya usajili pamoja na Mkuu wa Skauti Mels Daalder, tayari wameingia msituni kwa ajili ya kusaka nyota wapya kwa ajili ya kuboresha kikosi cha msimu ujao wa mashindano ikiwamo michuano ya 'Super League' inayotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu.

**Akizungumza na Nipashe jana, Robertinho alisema anahitaji kuimarisha kikosi chake katika usajili kwa kila nafasi kuwe na wachezaji wawili au zaidi wenye ubora na kiwango kizuri.**

"Msimu huu tumeshindwa kufikia malengo kwa sababu ya kukosekana kwa nyota wa kikosi cha kwanza kuumia na kushindwa kupata mbadala wao wenye uwiano mzuri na yule tuliyemkosa, tayari nimewasilisha ripoti na mapendekezo yangu, sasa ni muda wa kuandaa timu nzuri na imara kuhakikisha tunafanya usajili mkubwa kulingana na malengo yetu tuliyojiwekea," alisema Robertinho.

Aliongeza kuwa wanahitaji kubadilisha fikra za wachezaji na mipango yao kwa ajili ya msimu ujao ambao wamepania kurejesha makali yao.

Miongoni mwa majina yaliyopendekezwa, gazeti hili lilinasa jina la kipa wa Vipers FC ya Uganda, Alfred Mudekereza ametajwa kuwa katika mipango ya kocha Robertinho kwa msimu ujao.

Kipa huyo namba moja wa Vipers United ameonyesha kiwango kizuri katika michuano ya kimataifa na kupendekezwa kuwa miongoni mwa nyota watakaosajiliwa kwa msimu ujao wa mashindano.

Chanzo cha ndani kimesema kuwa Robertinho amewataka viongozi kuhusu suala la kipa walifanyie kazi mapema ili kuziba nafasi ya Beno Kakolanya ambaye taarifa zinasema nyota huyo atatimka Simba.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ibra Class azima tambo za Chino

Na Saada Akida

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Ibrahim Class juzi usiku alifanikiwa kumtandika bila 'utata' bondia Said Chino katika pambano la kuwania mkanda wa Taifa wa TPBRC lililopigwa juzi usiku.

Kabla ya pambano hilo la uzito wa 'Super Feather' lilifanyika kwenye ukumbi wa Warehouse jijini Dar es Salaam mabondia hao wote walitambiana kuibuka na ushindi, hata hivyo alikuwa Ibra Classic aliyefanikiwa kuzizima tambo za mpinzani wake.

Chino licha ya kujitahidi kujitafuta katika kila raundi kwa kutumia ngumi zake nzito lakini hazikuweza kufua dafu mbele ya Class aliyecheza kwa umakini mkubwa ambapo alitumia muda mwingi kumchapa kwa ngumi za 'jab' zilizokuwa zinamfikia kirahisi Chino kutokana na 'gadi' yake kuwa nyepesi.

Class amedhihirisha yeye ndiye mfalme katika uzani huo hapa nchini kwa sasa baada ya ushindi huo wa mpinzani wake anayeshika nafasi ya pili kwa ubora.

Majaji wote matatu kwenye pambano hilo walitoa ushindi kwa Class ambapo Jaji namba moja alitoa pointi 98-91, jaji namba mbili alimpa Class 97- 92 huku jaji namba tatu akimpa Class 97 dhidi ya 92 za Chino.

Akizungumza na Nipashe baada ya pambano hilo, Class alisema kuwa aliwaambia mapema Watanzania kuwa Chino siyo bondia mgumu kwake na kuwa aliamini angempiga kwenye pambano hilo.

"Niliwaambia Watanzania mapema kwamba huyu siyo bondia ni mpigadebe kwa sababu anaongea sana lakini nashukuru Mungu nimefanikiwa kushinda pambano hili, yeye anasema amenipiga ngumi nikadondoka ninachotaka kumwambia kuwa video zipo na kilichotokea kila mmoja ameona kwamba alinikanyaga nikashindwa kutembea," alisema Class.

Naye Chino alisema hana sababu ya kuongea sana kwa kuwa alichokifanya kila mmoja ameweza kukiona hadi kupelekea kumwangusha Class kutokana na kumpiga ngumi kali huku akitaka kupewa pambano la marudiano.

"Kweli Class ni bondia wakawaida sana na amekuwa akiletewa mabondia wepesi na ndiyo maana nimeweza kumwangusha na kila mmoja ameona, amecheza na Mmexico halafu Mzimbabwe nani ambaye amefanikiwa kumwangusha yeye atabakia kuwa ni bondia wa media, " alisema Chino.

## Nahodha KMC, Meridianbet watoa msaada

Na Saada Akida

NAHODHA na beki wa timu ya KMC FC, Sadala Lipangile, kwa kushirikiana na kampuni ya mchezo wa kubashiri wa Meridianbet, wametoa misaada mbalimbali kwa jamii inayomzunguka maeneo ya Goba jijini Dar es Salaam.

Beki huyo aliambatana na mkuu wa kitengo cha masoko na Mawasiliano cha Meridianbet, Matina Nkurlu na kutoa msaada kwa familia 10 ikiwamo mama mjane mwenye familia ya watu 19.

Msaada huo uliotolewa na beki huyo kushirikiana na Meridianbet ambao ni wadhamini wakuu wa timu ya KMC FC. Miongoni mwa vitu vilivyotolewa ni mafuta ya kupikia, mchele, sukari, sabuni pamoja na vifaa vya usafi.

Akizungumza na Nipashe jana, Lipangile amemshukuru Mungu kwa kumwezesha kufika katika eneo hilo pamoja na wadhamini wa timu yake, Meridianbet na kwenda kutoa alichojaliwa kwenye familia ya wanaoishi katika mazingira magumu na wajane.

Alisema ameamua kutoa kidogo kwa jamii yake kwa sababu ametoka kwenye maisha kama hayo na Meridianbet wamekuwa sehemu ya kufanikisha jambo hilo ambalo alitamani kulifanya muda mrefu sana.

## FA Cup Unguja kurindima leo

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

NUSU Fainali ya Michuano ya Kombe la ZFF (FA Cup) kwa kanda ya Unguja inatarajiwa kupigwa leo katika Viwanja vya Mau kisiwani hapo.

Nusu fainali ya kwanza itazikutanisha timu ya Black Sailor dhidi ya New King ambayo inacheza Ligi daraja la kwanza Kanda ya Unguja wakati nusu fainali ya pili utazikutanisha timu ya JKU dhidi ya Mwembe Makumbi City nayo kutokea Ligi daraja la kwanza.

Michezo yote itachezwa majira ya saa kumi alasiri katika Uwanja wa Mau A na Mau B.

Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano, Ali Bakar 'Cheupe' alisema maandalizi yote kuelekea hatua ya nusu fainali yamekamilika.

Alisema tayari kamati ya mashindano kwa kushirikiana na mdhamini wa haki ya matangazo wa michuano hiyo Zanzibar Cable TV imeweka mazingira ya michezo yote ambayo itachezwa siku moja ionyeshwa mubashara.

Alisema katika kuhakikisha kanuni zinafuatwa tayari kamati hiyo imeziita timu zote zilizotinga hatua hiyo ya nusu fainali ili kuwakumbusha kufuata kanuni ikiwamo kutojihusisha na vitendo vyovyote vitakavyoashiria upangaji wa matokeo.

## ZISIKUPITE

### RASHFORD KUONGEZA UNITED

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anatarajia mshambuliaji wa England, Marcus Rashford ataoongeza mkataba wake na klabu hiyo ya Old Trafford, 25, huku mkataba wa sasa wa mchezaji huyo ukikamilika mwishoni mwa msimu wa 2023-24. ***(Viaplay, viaManchester Evening News)***

### JUDE KUTUA REAL MADRID

REAL Madrid itamsajili kiungo wa kati wa England, Jude Bellingham, 19, kutoka Borussia Dortmund kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 87 pamoja na nyongeza za pauni milioni 21. ***(Sunday Mirror)***

### AMFIKIRIA LUKAKU

KOCHA mpya mtarajiwa wa Chelsea, Mauricio Pochettino anataka kumtathmini mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, 30, ambaye mkopo wake katika klabu ya Inter Milan kutoka unamalizika msimu huu wa joto, lakini mchezaji huyo anataka kusalia katika klabu hiyo ya Italia. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### NEVES AIVUTIA LIVER

LIVERPOOL imeomba kufahamishwa kuhusu hali ya kiungo wa Ureno, Ruben Neves, ambaye anaingia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake na Wolves na amekuwa akihusishwa sana na Barcelona. ***(Football Insider)***

### HEE-CHAN ATAZAMWA

KLABU za Aston Villa, Newcastle United, Tottenham Hotspur na AS Roma zinaweza kumtazama mshambuliaji wa Wolves mwenye umri wa miaka 27, Hwang Hee-chan kwani klabu hiyo ya Midlands inaweza kulazimika kuuza wachezaji ili kutimiza sheria za masuala ya fedha (FFP). ***(Sunday mirror)***

### SPURS YAMTAKA SOLOMON

KLABU ya Tottenham Hotspur inatafuta kumsajili winga wa Israel, Manor Solomon, 23, ambaye amekuwa akiichezea Fulham, baada ya Fifa kusema kuwa mchezaji huyo anaweza kuondoka Shakhtar Donetsk kwa uhamisho wa bure msimu huu wa joto. ***(Athletic)***

### BOEY ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inafikiria kumnunua beki wa kulia wa Ufaransa, Sacha Boey, 22, anayechezea klabu ya Galatasaray ya Uturuki. ***(SundayTelegraph)***

### ARSENAL ILIKATAA

KLABU ya Asenal ilikataa kuweka kipengele cha kuachilia huru katika mkataba mpya wa winga wa England, Bukayo Saka, 21 na badala yake wakampa mkataba mfupi kuliko ilivyotarajiwa, ambao utaendelea hadi mwaka 2027. ***(Mail on Sunday)***

### CARVALHO AFUATILIWA

KLABU ya Burnley inafuatilia hali ya kiungo mkabaji wa Liverpool, Fabio Carvalho, 20, na iko tayari kumchukua kwa mkopo wa kudumu Mreno huyo. ***(Football Insider)***

### ORIGI KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Divock Origi, 28, anatazamiwa kuondoka AC Milan na klabu za Uturuki zinamtaka mchezaji huyo. Lakini fowadi huyo wa zamani wa Liverpool angependelea kurejea katika Ligi Kuu ya England. ***(Il Corriere dello Sport)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AIPA UBINGWA PSG, AKIWEKA REKODI MPYA

**PARIS,** Ufaransa

●●● Goli lake la pekee lililoipa ubingwa timu yake lavunja rekodi ya 'mpinzani' wake...

PARIS Saint-Germain ilifanikiwa kutwaa taji la 11 la rekodi la Ligi Kuu ya Ufaransa baada ya kutoka sare ya 1-1 na Strasbourg siku ya Jumamosi na kuwazidi pointi nne Lens waliopo nafasi ya pili kukiwa kumesaliwa na mchezo mmoja.

**Mshindi wa Kombe la Dunia, Lionel Messi alifunga bao pekee kwa PSG akiunganisha pasi ya Kylian Mbappe dakika ya 59.**

Mshambuliaji wa zamani wa PSG, Kevin Gameiro, aliisawazishia Strasbourg dakika ya 79.

Lilikuwa bao la 496 kwa Messi kwenye Ligi Kuu barani Ulaya na kuvunja rekodi ya Cristiano Ronaldo ya kufunga mabao mengi kwenye ligi tano bora za Ulaya.

Lens ilijihakikishia nafasi ya pili na kuingia moja kwa moja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kwa kuifunga Ajaccio iliyoshuka daraja 3-0 nyumbani.

Mabingwa watetezi PSG waliwapita vigogo wa zamani wa Ufaransa Saint-Etienne, ambao walishinda taji lao la 10 mwaka 1981 lakini walishuka daraja la pili msimu uliopita.

"Kila kitu hakikuwa sawa, lakini taji hili ni la wachezaji. Kuwa mabingwa wa Ufaransa siku zote ni kitu, kwa mtazamo wa kibinafsi, ninaithamini sana kazi yao," alisema kocha Christophe Galtier.

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wake katika klabu hiyo baada ya kuinoa kwa msimu mmoja, Galtier alisema: "Nimekuwa nikisoma mambo mengi hapa na pale lakini kuna tofauti kati ya kile kinachoandikwa na kinachoendelea."

PSG wameshinda mataji tisa kati ya 11 tangu wafadhili wa Qatar QSI wachukue usukani miaka 12 iliyopita, na mara ya kwanza kati ya hayo mwaka 2013. Mataji mengine ya PSG yalikuwa mwaka 1986 na 1994.

"Bila shaka huu ni wakati wa kihistoria kwa Paris Saint-Germain. Ubingwa huu wa 11 wa ligi ya Ufaransa ni thawabu kwa kazi ngumu tuliyoifanya kwa miaka 12 iliyopita," alisema rais wa PSG Nasser al-Khelaïfi.

"Kuweka historia ya Ligue 1 na kuipita Saint-Etienne ni jambo la kujivunia." aliongezea kusema Nasser al-Khelaifi.

Ubingwa huo utaadhimishwa Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Parc des Princes wakati PSG watakapokaribisha Clermont katika mchezo unaotajwa kuwa wa mwisho kwa Messi kuichezea PSG.

Vyanzo viliiambia ESPN mapema mwezi huu kwamba Messi ataondoka PSG mkataba wake utakapomalizika msimu huu wa joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 ana ofa kutoka Saudi Arabia na klabu yake ya zamani ya Barcelona na klabu ya Ligi Kuu ya soka ya Marekani, Inter Miami vyanzo vilingeza.

Messi alizomewa na mashabiki wa PSG wakati fulani msimu huu baada ya kiwango chake kushuka kufuatia kurejea kwake kutoka kwenye ushindi wa Argentina kwenye Kombe la Dunia, na alisimamishwa na klabu mwezi huu baada ya safari isiyoidhinishwa kwenda Saudi Arabia.

Lakini mwishowe ni bao lake ndio lililowaruhusu mashabiki kusherehekea na kumpa Messi kombe kuu la 43 katika maisha ya soka ngazi ya klabu na nchi.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
BARNSLEY
VERSUS
SHEFFIELD WED
1 | 3.33
X | 3.28
2 | 2.11

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# SOUTHGATE AHOFIA NAFASI YAKE ENGLAND

**LONDON,** England

GARETH Southgate anajua michuano ya Euro ya mwakani inabidi iende vyema ili kuwe na "uwezekano machoni kwa mtu yeyote" kwake kusalia kama kocha wa England.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 52 alichukua mikoba baada ya kufukuzwa kwa Sam Allardyce mwaka 2016 na ameendelea kusimamia kipindi bora zaidi cha timu ya taifa.

England ilitinga nusu fainali ya Kombe la Dunia 2018 kabla ya kupoteza mchezo wa fainali ya Euro 2020 kwa mikwaju ya penalti na Italia kwenye uwanja wa Wembley.

Kulikuwa na dalili zaidi za maendeleo wakati timu hiyo ilipotolewa nje na Ufaransa kwenye Kombe la Dunia mwaka jana, lakini mwaka mgumu ulimfanya Southgate afikirie kama atamaliza mkataba wake hadi 2024.

Kocha huyo aliamua kusalia baada ya wiki moja ya kutafakari kufuatia kufanya vibaya Qatar, lakini michuano ya Ulaya msimu ujao inaweza kuthibitisha fainali zake za mwisho kuinoa England.

"Mkataba wangu ni hadi Desemba," alisema Southgate.

Mtazamo wa haraka wa England ni kuchukua hatua kubwa kuelekea Ujerumani kwa kuzishinda Malta na Macedonia Kaskazini mnamo Juni, lakini kwa wachezaji kadhaa mustakabali wao uko hewani.

# Baada ya ubingwa, Bayern yatimua watendaj

**MUNICH,** Ujerumani

SHEREHE za ubingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga za Bayern Munich ziligubikwa haraka na mkanganyiko wa uamuzi wa klabu hiyo kuwatimua mlinda mlango wa zamani, Oliver Kahn na Hasan Salihamidžić kutoka nyadhifa zao kama watendaji wakuu.

Bayern walipata ubingwa wa Ujerumani katika dakika za mwisho za msimu Jumamosi huku Jamal Musiala akifunga bao la ushindi wa 2-1 dhidi ya Cologne na hivyo kumaliza mbele ya Borussia Dortmund kwa tofauti ya mabao.

Muda mfupi baadaye, klabu ilitangaza bodi yake ya usimamizi imeamua kumfuta kazi Kahn kama mtendaji mkuu na Salihamidžićmkurugenzi wa michezo mara moja.

"Badala ya kusherehekea, sasa tuna suala linalofuata," kocha wa Bayern Thomas Tuchel alisema.

Wote Kahn na Salihamidžić walikuwa chini ya shinikizo kufuatia kuporomoka kwa Bayern msimu huu.

Mbio za kuwania taji la Bundesliga zilikuwa za karibu zaidi kwa miaka mingi baada ya Bayern kushinda kwa raha miaka 10 ya awali, huku wakitolewa kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Ujerumani.

Rais wa klabu, Herbert Hainer baadaye alisema uamuzi wa kuwatimua watu hao wawili ulifanywa Ijumaa kabla ya timu hiyo kupata mafanikio



yasiyotarajiwa ya Bundesliga.

Dortmund walikuwa wanaongoza kwa pointi mbili kuelekea mechi ya mwisho na walihitaji tu kuifunga Mainz nyumbani Jumamosi ili kuwa na uhakika wa kuwa mabingwa wa Ujerumani. Badala yake, walitoka sare ya 2-2.

Salihamidžić alikuwa Cologne kwa mechi ya mwisho ya Bayern, lakini Kah hakusafiri.

"Sikuruhusiwa na klabu Kahn aliandika kwenye Twter, akipinga madai ya klab kwamba alikosa mchezo kw maagizo ya daktari.

Tuchel alionekana kusha gazwa na uamuzi wa klab hiyo kuwafuta kazi wa waliomleta kwenye klab kama mbadala wa Julian N gelsmann Machi.

"Nilijua kuhusu hilo tang jana (juzi). Wawili hao wa husika kwa kiasi kikubwa n ukweli kwamba tulienda s fari hii pamoja. Ndiyo maan ni lazima nilifanyie kazi sasa alisema Tuchel baada ya us indi wa timu yake. "Laki nadhani nitaendelea na safa yangu hapa Bayern."

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# BODI YA LIGI KUU YAZIOMBA RADHI KLABU LIGI KUAHIRISHWA

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara imeziomba radhi klabu zote, zikiwamo zile zilizoguswa na kuahirishwa kwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kuipisha Yanga kucheza michezo miwili ya fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (CAF), dhidi ya MC Alger ya Algeria.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Almasi Kasongo, alisema bodi hiyo inaomba radhi kwa usumbufu kwa klabu pamoja na gharama ambazo baadhi ya klabu imezipata kutokana na kuahirishwa kwa mechi hizo.

**Hata hivyo alisema hizo zote ni changamoto ambazo ziko nje ya uwezo wao, kwani wakati wanapanga ratiba ya Ligi Kuu, Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika lilikuwa bado halijaweka wazi fainali ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.**

Hali hii inakuja kutokana na taarifa kuwa tayari timu ya Polisi Tanzania ilikuwa njiani kwenda Dar es Salaam kucheza mechi dhidi ya Simba iliotarajiwa kuchezwa Mei 24 lakini taarifa ya kuahirishwa iliwakuta wakiwa njiani.

“Changamoto iliyojitokeza ni kwamba wakati sisi tunapanga ratiba, wenzetu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika walikuwa hawajaweka wazi ni lini fainali za Ligi ya Mabingwa na Shirikisho zitachezwa, kwa hiyo wakati sisi tunatoa ratiba zetu za mashindano yetu ya ndani, baadaye wakaja kutangaza tarehe za michezo hiyo ya fainali ya Kombe la Shirikisho itachezwa Mei 28 na ya marudiano Juni 3,” alisema Kasongo.

Alisema wao walitamani kuendelea na ligi ili Yanga ikimaliza mechi zake nayo imalizie, lakini kwa sababu raundi zote mbili zilizobaki ni za maamuzi zinazoweza kuishusha timu daraja, wanahitaji usawa kwa timu zote.



Mshambuliaji wa Yanga, Kennedy Musonda (katikati), akitafuta mbinu ya kuwatoka mabeki wa USM Alger katika mchezo wa jana wa fainali ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Robertinho aahidi

INATOKA UK. 24

Misri, Morocco, Tunisia kote wanaizungumzia,” alisema kocha huyo.

Mipango na maneno ya kocha huyo inafanana sana na maoni ya wanachama na mashabiki wa Simba kuwa kikosi chao ni finyu, kina wachezaji wachache wenye uwezo wa hali ya juu kiasi cha kuweza kupambana na klabu yoyote Afrika na kushinda, lakini nusu ya kikosi kilichobaki ambacho kingewasaidia wenzake kina wachezaji ambao huenda wasiweze hata kuingia nne bora ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Msimu huu Simba imetoka kapa katika kila mashindano waliyoshiriki, kwa mara ya pili mfululizo wameshuhudia ubingwa wa ligi kuu ukienda kwa wapinzani wao wakubwa, Yanga, lakini wameondolewa kwenye hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho la TFF (FA) huku pia wakiishia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## *Haijaisha...*

INATOKA UKURASA 24

kiruka ukuta wa uzio wa Uwanja wa Mkapa. Polisi walilazimika kutumia nguvu kuwadhibiti.

Milango ya uwanja huo ilifunguliwa saa tano asubuhi lakini wakati huo tayari kulikuwa na kundi kubwa la mashabiki waliokuwa wamesubiri kuingia.

Wingi wa mashabiki ulisababisha mashabiki hao kuvunja mageti mawili ya uwanja kutokana na wahusika kuchelewa kuyafungua huku askari wakishindwa kuwadhibiti kutokana na wingi huo.

Hadi kufikia saa 6:30 mchana, eneo la nje ya uwanja huo lilikuwa limeshafurika mashabiki waliokuwa wamevaa jezi za rangi ya kijana na njano.

Jana jioni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa alichokiita taarifa za awali kuhusu majeruhi wa vurugu hizo. Alibainisha kuwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Temeke ilikuwa imepokea majeruhi 30, huku mmoja akifariki dunia.

Alifafanua kuwa aliyefariki dunia ni mwanamume mwenye umri unaokadiriwa miaka 40. Alisema “...majeruhi wengi wanaendelea vizuri. Wana majeraha madogo madogo. Wanaendelea na vipimo.”

Ummy alisema kuwa timu kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ilikuwa uwanjani, ikifuatilia kwa karibu kuangalia kama kulikuwa na majeruhi wengine.

Pia timu ya wataalamu wa huduma za dharura ya Hospitali ya Rufani ya Taifa Muhimbili (MNH) iliwasiliana na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Temeke na ilikuwa tayari kuwapokea na kutoa huduma kwa majeruhi wanaohitaji matibabu zaidi.


## MECHI ZA USHINDI

“1” - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
“X” - NI TIMU KUTOKA SARE
“2” - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 29/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 5486 | Changchun Yatai vs Shanghai SIPG | 4.61 | 3.53 | 1.64 |
| 15:00 | 1696 | Lyngby vs Aalborg | 2.83 | 3.64 | 2.24 |
| 15:00 | 2687 | AFC Leopards vs Nairobi City Stars FC | 1.75 | 3.30 | 4.10 |
| 15:00 | 2761 | Vorskla Poltava vs Kolos Kovalivka | 1.94 | 3.19 | 3.55 |
| 15:00 | 2859 | FC Metalist 1925 vs FC Kryvbas Kriviy Rih | 3.49 | 3.08 | 2.00 |
| 15:00 | 2890 | Silkeborg vs Midtjylland | 3.29 | 3.64 | 2.01 |
| 15:00 | 3983 | Ethiopian Medhin vs Wolkite City FC | 1.58 | 3.68 | 5.08 |
| 15:00 | 4553 | Dynamo Kiev vs Veres Rivne | 1.30 | 4.72 | 7.60 |
| 15:00 | 5186 | FC Metalist Kharkiv vs FC Minaj | 3.38 | 3.33 | 1.95 |
| 15:00 | 5274 | FK Lviv vs FC Ingulets | 5.98 | 3.66 | 1.49 |
| 15:00 | 5729 | Chernomorets Odessa vs Rukh Vinnyky | 2.04 | 3.08 | 3.39 |
| 16:00 | 1056 | Bryne vs Kfum Oslo | 2.21 | 3.29 | 2.83 |
| 16:00 | 1170 | Moss vs Raufoss | 2.20 | 3.24 | 2.88 |
| 16:00 | 1772 | Fredrikstad vs Aasane Fotball | 1.62 | 3.64 | 4.61 |
| 16:00 | 2479 | Jerv vs Hodd | 2.01 | 3.19 | 3.35 |
| 16:00 | 3928 | Levanger vs Strommen | 1.43 | 4.32 | 5.56 |
| 16:00 | 4161 | Kongsvinger IL vs Sogndal | 2.03 | 3.43 | 3.07 |
| 16:00 | 4783 | Mjondalen vs Sandnes Ulf | 2.28 | 3.35 | 2.68 |
| 16:00 | 5544 | IK Start vs Ranheim | 2.06 | 3.55 | 2.93 |
| 16:00 | 5682 | Kristiansund vs Skeid Fotball | 1.49 | 4.22 | 4.94 |
| 17:00 | 2616 | Viborg FF vs Copenhagen | 2.89 | 3.50 | 2.26 |
| 17:00 | 4208 | Barnsley vs Sheffield Wed | 3.33 | 3.28 | 2.11 |
| 17:30 | 1047 | St. Gallen vs FC Sion | 1.57 | 4.30 | 4.61 |
| 17:30 | 3289 | FC Zurich vs FC Lugano | 2.56 | 3.32 | 2.55 |
| 17:30 | 3454 | BSC Young Boys vs FC Winterthur | 1.28 | 5.46 | 8.20 |
| 17:30 | 3736 | FC Luzern vs Servette Geneva | 2.56 | 3.57 | 2.41 |
| 17:30 | 5425 | FC Basel vs Grasshoppers | 1.75 | 3.83 | 3.94 |
| 18:00 | 1549 | Stabaek vs Valerenga | 2.45 | 3.21 | 2.74 |
| 18:00 | 2129 | Bodo Glimt vs Viking | 1.42 | 4.62 | 6.10 |
| 18:00 | 3214 | Hadiya Hosahina FC vs Ethiopia Bunna SC | 2.44 | 2.85 | 2.95 |
| 18:00 | 3719 | Haugesund vs Tromso | 2.32 | 3.06 | 3.06 |
| 18:00 | 4010 | Molde vs Sandefjord | 1.22 | 6.08 | 10.27 |
| 18:00 | 4315 | Brann vs Rosenborg | 1.39 | 4.52 | 6.94 |
| 18:00 | 4360 | Sarpsborg vs Aalesunds | 1.53 | 3.99 | 5.47 |
| 18:00 | 5022 | Odd Ballklubb vs Stromsgodset | 1.84 | 3.67 | 3.73 |
| 19:00 | 3506 | El Ittihad Alexandria vs Pyramids | 4.02 | 3.42 | 1.84 |
| 19:00 | 5299 | Brondby vs Nordsjalland | 3.29 | 3.85 | 1.96 |
| 20:00 | 2451 | Hammarby vs IFK Varnamo | 1.47 | 4.05 | 5.53 |
| 20:00 | 4281 | Degerfors vs Varbergs Bois | 1.87 | 3.38 | 3.59 |
| 20:10 | 4545 | BK Hacken vs IFK Goteborg | 1.37 | 4.60 | 6.14 |
| 20:15 | 4021 | Ham-Kam vs Lillestrom | 3.47 | 3.37 | 2.00 |
| 21:00 | 5085 | AL Qaisoma vs AL Riyadh | 3.35 | 3.14 | 2.03 |
| 21:30 | 2803 | UAI Urquiza vs Comunicaciones | 3.01 | 2.90 | 2.36 |
| 21:30 | 5191 | Al Ahly Cairo vs Ceramica Cleopatra | 1.58 | 3.73 | 5.44 |
| 21:30 | 5331 | CA Atlas vs Berazategui | 2.21 | 2.89 | 3.31 |
| 22:00 | 2831 | Vaca Diez vs Oriente Petrolero | 1.96 | 3.36 | 3.41 |
| 22:00 | 3938 | FUS Rabat vs FAR Rabat | 2.31 | 2.88 | 3.03 |
| 22:00 | 4290 | Always Ready vs The Strongest | 2.53 | 3.32 | 2.48 |
| 22:00 | 4625 | Wydad Casablanca vs Maghreb Tetouan | 1.34 | 4.10 | 8.20 |
| 22:30 | 2110 | Colon Santa Fe vs Central Cordoba | 1.97 | 3.22 | 3.53 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Mei 29, 2023
Nipashe



Southgate ahofia nafasi yake England UKURASA 22



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (katikati), akiwatoka mabeki wa USM Alger katika mchezo wa fainali ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika, Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# HAIJAISHA...

## ●●● Mayele afunga goli la ajabu, mvua yaharibu mipango...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HISTORIA ya huzuni ya mwaka 1993 ilijirudia jana baada ya wawakilishi wa Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho, Yanga kuchapwa mabao 2-1 na Union Spotive de la Medina Alger ya Algeria katika mechi ya kwanza ya fainali kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**Magoli ya Aymen Mahious kipindi cha kwanza na Islam Merili kipindi cha pili ndiyo yaliyowatonesha Watanzania kidonda cha mwaka 1993, Simba ilipofungwa 0-2 na Stella Abidjan ya Ivory Coast katika fainali ya michuano hiyo wakati huo ikitwa Kombe la CAF.**

Michuano hiyo ilibadilishwa jina na kuwa Kombe la Shirikisho mwaka 2004. Mechi ilichezwa Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru) baada ya mchezo wa kwanza ugenini Simba kulazimisha suluhu.

Rekodi za Yanga msimu hizo ndizo zinazotoa matumini 'haijaisha' kwa kuwa. Sasa itatakiwa 'kupindua meza' ugenini watakaporudiana Juni 3 katika mechi ya pili fainali.

Mshambuliaji Fiston Mayele aliwarudisha mashabiki wa Yanga katika shangwe dakika ya 82 baada ya kusawazisha kwa bao la ajabu, akipokea pasi ya kichwa ndani ya eneo la boksi kutoka kwa Mudadhir Yahaya. Kwa utulivu mkubwa, aliutuliza mpira kisha kuachia shuti kali la mguu wa kulia, kimo cha kuku.

Ni goli lililoamsha matumaini kwa wanajangwani waliokuwa na huzuni baada ya kutanguliwa kufungwa kwa bao la kichwa la Mahious dakika moja baada ya nusu saa ya mchezo. Lilitokana na mpira wa adhabu ndogo baada ya Brahim Benzaza kuangushwa pembeni mwa lango la Yanga.

Hata hivyo, furaha ya watoto wa Jangwani ilidumu kwa dakika mbili tu huku mvua nayo ikiwaongeza uchungu baada ya mshambuliaji Islam Merili kuipatia USM Alger bao la pili na la ushindi. Wageni walianza vizuri ndani ya boksi la Yanga.

Mfungaji hakuwa amezongwa na mshambuliaji yeyote wa Yanga alipopokea pasi murua kutoka kwa Khaled Bousseliou. Akamtungua kipa Djigui Diarra.

Katika robo saa ya kwanza ya mchezo, Yanga ilifanya shambulizi kali, Mayele na Kennedy Musonda walipowatoka mabeki wa USM ALger na kumpa pasi ya upendo Tuisila Kisinda aliyekuwa amebaki na kipa Oussama Benbot lakini akapiga shuti mtoto lililoishia mikononi mwa kipa huyo.

Mfungaji wa bao la kwanza, Mahious, pia alikaribia kufunga la pili dakika tano kabla ya saa ya mchezo baada ya kuupata mpira pembeni kidogo mwa boksi, akawalamba chenga mabeki wa Yanga kabla ya kupiga shuti kwa mguu wa kushoto, lakini Diarra akafuta makosa ya mabeki wake.

Ni shambulizi lililojibiwa na Yanga dakika moja baadaye, Kisinda alipoambaa na mpira akipita winga ya kulia na kumpasia Stephane Aziz Ki ambaye alipiga shuti lilitoka nje kidogo na kugusa nyavu.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi alifanya mabadiliko ya mkupuo, kwa kuwaingiza Bernard Morrison, Joyce Lomalisa na Djuma Shaaban na baadaye akamwingiza Clement Mzize na kuipa nguvu timu kwa kiasi kikubwa kusukuma mashambulizi langoni mwa USM Alger.

Bao la Mayele ni la saba kwake katika michuano hiyo na anaongoza akiwa na nafasi kubwa ya kuibuka kuwa mfungaji bora katika michuano hiyo msimu huu.

**VURUGU, KIFO**

Kabla ya mechi hiyo kuanza, kulikuwa na vurugu za mashabiki waliolazimisha kuingia uwanjani, baadhi wa-

INAENDELEA UKURASA 23

## Robertinho aahidi kuiandaa Simba ya makombe

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Roberto Oliveira, ameweka wazi kuwa licha ya kupokea ofa nyingi kutoka klabu za nje ya nchi, amezikataa na amejipanga kuiandaa Simba itakayokuwa na makali yatakayowawezesha kutwaa makombe mbalimbali.

Robertinho amesema bado hajamaliza kazi yake ndani ya Simba na lengo lake ni kuisuka timu hiyo na kuifanya kuwa tishio ndani na nje ya nchi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, kocha huyo alisema kwa sasa timu yake inahitaji mabadiliko makubwa na pia fikra za wachezaji zinatakiwa zibadilike kwani amegundua kuwa Simba ni klabu kubwa sana Afrika.

"Simba ni timu kubwa lakini tunahitaji nini? Kwa wakati huu tuibadili timu yetu, tunatakiwa kubadili mipango yetu, fikra za wachezaji, nadhani sasa ni muda mzuri wa kuandaa timu yetu, inabidi tuandae timu imara, kuna ofa nyingi zimekuja kwangu lakini nimeamua kubaki hapa, napenda kila kitu nina furaha kwa ajili ya watu wa Tanzania, wanapenda sana mpira na wanapenda timu yao, baada ya kupokea maombi mengi nimeamua kubaki hapa nataka nibaki nitengeneze kikosi kizuri na cha kutisha kitakacholeta upinzani mkubwa Afrika," alisema.

Alisema lengo lake ni kutengeneza kikosi kitakachokuwa na wachezaji wawili wawili kwenye kila nafasi huku wakiwa na uwezo sawa kwani kwa sasa wasipokuwapo baadhi ya wachezaji, timu inapwaya.

"Nataka kila nafasi iwe na wachezaji angalau wawili ambao hawapishani sana, kama Saido hachezi, Mzamiri kama hachezi, wawepo wachezaji wengine kama wao wanaoweza kuanza kwenye kikosi, Simba inatakiwa iwe na kikosi imara, kwa sababu ni timu kubwa inayozungumzwa sana, hata

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >